

KILE KINACHOHITAJIKA

KUSHINDA KUTOKUAMINI

KWOTE: IMANI YETU



Nimetazamia kwa muda mrefu nafasi hii adhimu na tukufu kuja kwenye—kwenye jiji hili, kuwahudumia watu hawa wapendwa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Yapata, katika siku tangulizi za mwanzoni, nilipomtuma Bw. Lindsay, moyoni mwangu nilikusudia, “Yakima,” nami nikaishia Spokane. Kwa hiyo basi tena, nilituma mtu Yakima, na kwa namna fulani mkarukwa tukaenda mahali pengine. Kwa hiyo, usiku wa leo, huku ni kungojea kwa muda mrefu, yapata miaka kumi ama kumi na miwili nimetazamia fursa ya kuja kwenye jiji hili.

² Nina furaha sana kwa ajili ya fursa hii pia, ya kupata shule hii nzuri hapa, iliyopewa jina la Rais wetu mpendwa, Dwight Eisenhower. Nami ninatumaini ya kwamba Bwana atatupa mengi sana, kwa wingi kuliko yote ambayo tungeweza kufanya ama kuwazia, siku hizi kumi za ibada. Nasi tunamtaka Mungu, kama ni mpango Wake mkuu, kuokoa kila mtu aliyepotea aliyeko katika nchi hii, papa hapa, mahali hapa aokolewe.

³ Kweli ninaamini ya kwamba kuja kwa Bwana Yesu kumekaribia. Ninaamini hilo, kwa kuwa tunaishi katika vivuli vya kuja Kwake, nami ninataka kufanya yote nijuayo kumweka kila mtu tayari kwa ajili ya tukio hilo kuu ambalo limetabiriwa, na watu wamelitazamia tangu kuondoka Kwake. Nasi tunaona hali zikitokea, katika ulimwengu wa kisiasa, na pia katika ulimwengu wa kijeshi, na katika ulimwengu wa kidini, kwamba ishara zote zinaelekeza sasa kwamba kule Kuja kumekaribia. Tunaona Kanisa katika uchache, waaminio wa kiroho, pia tunaona ninii, yote aliyonena habari zake yakitukia.

⁴ Tunajua ya kwamba yanayotungojea ni mabomu kutoka mahali popote ulimwenguni sasa, si lazima wayaangalie mataifa makubwa, mataifa madogo yana makombora ya kuuangamiza ulimwengu wakati wowote watakao; na makombora hayo yako mikononi mwa watu wenye dhambi. Na kila skrini ya rada imewekwa, ikingojea, ikingojea moja liingie kwenye skrini yao, nayo yakiingia, watarusha yao. Itakuwaje yote yatakapotukia namna hiyo?

⁵ Nina furaha sana kwamba ninajua Bwana Yesu ni Mwokozi wangu. Nina furaha sana kwa hilo! Nina furaha sana ya kwamba ninajua ya kwamba kuna makumi ya maelfu ya wengine

wanaojisikia kama ninavyojisikia, wanaungojea wakati huo mkuu.

⁶ Tunajua tu maisha jinsi tunavyoyajua, kama mwanadamu, kwa sababu hatujawahi kuwa chochote ila wanadamu, lakini tunapozaliwa mara ya pili, kuna Uzima utokao Juu, unaoingia ndani yetu.

⁷ Nimekuwa na majaliwa ya kusafiri mataifa mengi, kuona watu wengi, kwa jumla, nadhani, mara nyingi tumeizunguka dunia. Nimekuwa karibu kila taifa ulimwenguni, nikifanya umishenari. Nami ninaona, ninapoingia kwenye taifa, jambo la kushangaza ni kwamba taifa hilo lina roho fulani, roho hiyo ya taifa hilo inaonekana kama, kulitawala hilo taifa.

⁸ Tukienda Ujerumani, na si kama roho iliyo katika Ufini; tukienda Ufini, si kama roho iliyoko Australia; na ukienda Australia, si kama roho iliyoko Japani; halafu ukirudi Marekani, kuna roho ya Kimarekani. Kila mahali uendapo, unakuta roho tofauti, watu wanaishi tofauti, wanatenda tofauti. Lakini jambo moja kuu nimeona, ukimchukua Mjerumani na kumtuma Marekani, upesi ataichukua roho ya Marekani; ukimchukua Mmarekani, umtume Ujerumani, anachukua roho ya Ujerumani, bali popote na taifa lolote unaloenda, ukiwaona Wakristo waliozaliwa mara ya pili, wote ni sawa haidhuru ni wapi.

⁹ Nami nimewaona watu, wanaokuja mkutanoni, kama vile katika . . . Umati wetu mkubwa kuliko wote tuliopata kuwa nao ulikuwa ni laki tano huko Bombay, na halafu nakisia, wito wangu mkubwa sana wa madhabahuni, tuliopata kuhesabu ulikuwa huko Durban, Afrika Kusini, elfu thelathini, alasiri moja ya makafiri, walimpa Bwana Yesu mioyo yao, walipoona jambo fulani likitukia jukwaani, Waislamu elfu kumi walifuata hilo.

¹⁰ Sasa, lakini nimeona, hebu mchukue mtu wa mwituni na mtu wa kikabila wanaoingia ambao hata wasingejua ni upi mkono wa kulia na wa kushoto, hawavai nguo zozote, hawajui hata neno moja la Kiingereza, hawajui lolote, ila tu lugha yao ya kikabila, lakini wanapompokea Roho Mtakatifu, wanatenda na kufanya mambo yale yale mnayofanya mnapompokea Roho Mtakatifu, wanatenda tu vivyo hivyo, wanaenda vivyo hivyo kabisa. Inaonyesha ya kwamba Mungu ni wa ulimwengu mzima. Mungu yuko kila mahali, anajua yote, hana kikomo, Naye hufanya kazi vivyo hivyo na watu Wake wote.

¹¹ Na kila mwanadamu, bila kujali rangi, ama kile alichu, jinsi alivyo mdogo, jinsi alivyo mkubwa, ana rangi gani, wote ni wa damu moja, Mungu alifanya kwa mataifa yote, damu moja. Mjerumani, Mswisi, Mwafrika, kila mtu anaweza kumpa mwenzake nyongeza ya damu, rangi ya ngozi yetu, na ukubwa wetu hauna uhusiano wowote nalo.

¹² Lakini kila mwanadamu ana chumba kidogo moyoni mwake, ambamo hata hamna chembechembe ya damu ndani yake. Miaka mingi iliyopita wakosoaji walikuwa wakisema, “Mungu alifanya kosa baya sana aliposema, ‘Mtu aonavyo moyoni mwake,’ kwa sababu hakuna uwezo wa kiakili moyoni kwake kuwazia.”

¹³ Lakini miaka miwili iliyopita, ninaamini ndivyo, nilipokuwa Chicago katika mkutano, vichwa vikuu vya habari vilikuja gazetini, kwamba wamegundua, sayansi imegundua, ya kwamba mtu kweli ana uwezo wa akili moyoni mwake, kwamba kuna chumba kidogo moyoni, moyo wa mwanadamu, ambacho hakiko kwenye mo—moyo wa mnyama. Walikipata kwa utafiti wa moyo, na humo ndani wanasema ndipo mahali ambapo nafsi huishi. Kwa hiyo basi, hata hivyo, Mungu alikuwa sahihi aliposema, “Mtu aonavyo moyoni mwake.”

¹⁴ Sasa, tu—tunahoji kwa nia zetu, bali moyo hautoi hoja, moyo huamini tu. *Tunaangalia* kwa macho yetu, lakini *tunaona* kwa moyo wetu. Unaangalia...? Unasema, jambo fulani gumu, unasema, “Kamwe silioni.” Unamaanisha hulelewi, unaona, ufahamu wako unatoka moyoni mwako, una ufahamu wako.

¹⁵ Sasa, mara nyingi, ninajua Wakristo wote wanajua jambo hili, kwamba watu watawazia, “Vema, kamwe haliwezi kutukia, lakini hata hivyo, moyoni mwangu kuna kitu *fulani* kinachoniambia, kwamba litatukia.” Je, mumewahi kuwa na tukio hilo, ninyi Wakristo? Hakika, mumekuwa nalo. Huyu ni yule mtu wa ndani akiwazia, anatupilia mbali hoja, hana uhusiano wowote na hoja, kwa sababu kwa Mungu, maneno hayapaswi kuhojiwa. Hatuwezi kumhoji Mungu. Mungu kamwe hajulikani kwa sayansi, kamwe Mungu hajulikani kwa—kwa nguvu za akili, Mungu anajulikana tu kwa imani. Maarifa kamwe hayatampeleka mtu kwa Mungu, maarifa humpeleka mbali na Mungu.

¹⁶ Hapo ndipo ilipoanzia katika bustani ya Edeni. Kulikuwa na miti miwili, mmoja ulikuwa ni Mti wa Uzima, huo mwingine Mti wa Maarifa. Mwanadamu aliama kwanza kutoka kwenye Mti wa Maarifa, akajitenga na Mti wa Uzima. Na kila wakati anapouma Mti huo wa Maarifa, anaendelea kwenda mbali zaidi na Mti wa Uzima, kwa sababu anaanza kuwazia kwamba anajua jinsi ya kulihoji. Huwezi kumhoji Mungu, huna budi kurudi kwenye ule Mti rahisi wa Uzima, na kukaa chini pale, ukila tunda la Uzima.

¹⁷ Hilo ndilo lililotuleta hapa, kuwaletea ninyi watu hapa Yakima huduma ambayo Bwana amenipa. Na wengi wenu mlihudhuria mikutano mahali pengine, lakini kwa mji huu, labda, kuna wengi hapa juma hili ambao hawajawahi kuwa mikutanoni.

¹⁸ Sasa, mara nyingi watu husema, “Ndugu Branham, unaonyesha uponyaji wa Kiungu.” La, hilo ni kosa, ninamwonyesha Yesu Kristo. Mnaona? Uponyaji wa Kiungu ni

jambo dogo, wala kamwe huwezi kulifanya kubwa jambo dogo. Naye Kristo ndiye Somo letu kuu, basi tunaamini ya kwamba Kristo, Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, ya kwamba alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kisha akafufuka tena siku ya tatu, kulingana na Maandiko, na sasa ameketi mkono wa kuume wa ukuu wa Mungu, akiwa ni Kuhani Mkuu, kufanya maombezi tunapokiri.

¹⁹ Tu—tunangojea, tukimtarajia kuondoka Utukufuni siku moja kurudi duniani, kuwafufua wafu, na kuwahamisha wale walio hai katika mwili uliotukuka wapate kunyakuliwa angani, kuishi pamoja Naye kwa muda wa miaka mitatu na nusu, katika wakati wa ile dhiki, na kurudi kwenye dunia iliyosafishwa kuishi miaka elfu moja hapa duniani pamoja na Kanisa Lake, na kuwa pamoja Naye milele wakati atakapoketi katika kiti cha enzi cha Daudi. Sasa, tunaatazamia wakati huo mkuu.

²⁰ Basi somo letu katika maska- . . . katika ibada zetu ni *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*, yeye yule. Sasa, tunaamini Yeye ni yeye yule katika kila kanuni. Sasa, Waebrania 13:8 ndiyo mada yetu, msisahau jambo hilo sasa, wakati wa hii mikutano. Kama jambo lolote likiibuka isivyostahili, shikilia moja kwa moja kwenye Andiko hilo, na ulirudishe kwenye Maandiko. Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.

²¹ Sasa, hatuwezi kuyakana Maandiko, kwa kuwa Yesu alisema Maandiko yote, tunajua, yametolewa kwa uvuvio, na Mbingu na nchi zitapita, bali hakuna hata Andiko moja litakalopita, maana ni Neno la Mungu.

²² Sasa, tunaamini ya kwamba Mungu anaweza kufanya mambo ambayo hajayaandika katika Neno Lake, bali tunapenda kudumu tu na yale aliyoandika, ndipo tunajua tuna hakika, kama ukidumu tu na yale aliyoandika katika Neno.

²³ Sasa, katika siku hizi kumi, Mungu akituruhusu kuendelea, huenda ukaona—ukaona baadhi ya mambo yatakayoonekana yasiyo na maana kwako, lakini kama linaonekana ni swali dogo, katika kunena kwangu daima nitadumu moja kwa moja katika Maneno juu ya ahadi za Mungu. Hilo linatosha kwetu, kama tukidumu moja kwa moja na ahadi Zake, kama Mungu atathibitisha ahadi Zake zote, hilo ndilo tu tunalohitaji. Hivi hamwoni hivyo? Hilo ndilo tunalohitaji, kama Mungu atadumu na ahadi Zake.

²⁴ Kwa sababu ninaamini ya kwamba tunaishi katika siku ambayo kuna mambo ya kisiri yanayoendelea, na yataendelea kusonga mbele, na kuwa na utata, kwa sababu tunajua kwamba kutakuwako na Yane na Yambre watakaoinuka katika siku za mwisho kushindana na Musa na Haruni, kama Biblia ilivyosema, na uigaji fulani kutenda kana kwamba ni kitu ambacho sicho, bali Neno la Mungu daima ni kweli. Daima ninashikilia hilo, na, kwamba Neno la Mungu daima ni kweli Milele.

25 Wala hakuna neno la mtu, ama, hakuna mtu aliye bora kuliko neno lake. Nisipotimiza neno langu, basi mimi si kitu; na kama Mungu hatimizi Neno Lake, Yeye si Mungu. Lakini kama kweli Mungu hutimiza Neno Lake, basi daima Yeye anabaki Mungu. Ili awe Mungu, hana budi kulitimiza Neno Lake, mnaona, hana budi kulitimiza Neno Lake.

26 Na sasa, juu ya hizi... Labda usiku wa leo, ningetaka kuzungumza nanyi kwa muda kidogo, na kwa namna fulani tulijue jumba la mikutano, pamoja na watu, na kwa namna fulani tujiandae kwa ibada zijazo. Sasa, nilizungumza dakika chache zilizopita, ya kwamba hatukujaribu kuufanya uponyaji wa Kiungu jambo kubwa, hata hivyo tunafundisha hiyo kuwa moja ya kweli za Biblia, kwamba Yesu Kristo *alijeruhiwa* kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*.

27 Sasa, baraka zote za ukombozi kwetu, jamii ya binadamu, zililipiwa, kwa ajili yetu, pale Kalvari wakati Yesu alipokufa kwa ajili yetu. Tunaamini ya kwamba kazi na mpango mkamilifu wa Mungu, kila baraka ya ukombozi ilikamilishwa pale Kalvari, kwamba ahadi zote za Mungu zilifanywa kuwezekana kwa kila mwanadamu ambaye angezikubali wakati Yesu alipokufa ili kumsafisha mwanadamu mbele za Mungu pale Kalvari. Ninaamini ya kwamba kila mtu ulimwenguni aliokolewa wakati Yesu alipokufa pale Kalvari; kila mgonjwa ulimwenguni aliponywa wakati Yesu alipokufa pale Kalvari, lakini sasa, ni kazi iliyomalizika.

28 Sasa jambo la kufanya ni, je, tunaweza kuwafanya watu waone jambo hilo na kulikubali? Kwa hiyo, uponyaji wa Kiungu hautegemei kitu fulani cha kimazingaombwe, ambacho mtu fulani anacho mikononi mwao, ama mafuta fulani matakatifu, ama maji wanayowanyunyizia watu. Siamini mambo hayo, ni—ninaamini ya kwamba Damu ya Yesu Kristo inatosha kwa kila kitu tunachohitaji. Mnaona? Nami ninaamini ni kitu ambacho tayari kimelipiwa.

29 Sasa, njia ya kwanza na ya asili ya kupokea baraka zozote za ukombozi ni kwa kusikia Neno la Mungu, kwa sababu imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu, kama wahudumu wanavyohubiri. Kama hiyo ingekuwa mimi na wewe, hilo lingetosha, kama watu hawakutaka kutuamini, mbona, tungewaacha tu waendele. Lakini Mungu ni mwema sana, na mwingi wa rehema, hata baada ya yote hayo akatuma Neno Lake, kisha akatuma karama Kanisani, sote tumeamini hilo. Wakorintho wa Kwanza 12, kuna karama tisa za kiroho Kanisani, hizo zimo katika kila kanisa la mahali hapo, ama zinapaswa kuwa katika kila kanisa la mahali hapo, karama za uponyaji, karama za hekima, karama za maarifa, na karama ya, karama hizi zingine zote zimo Kanisani. Karama tisa mbalimbali za kiroho zimo katika kila kanisa la mahali.

³⁰ Halafu Mungu ana karama ambazo ametangulia kuzijua kwa ajili ya kila wakati na ameziweka Kanisani. Sasa, tunaona kuna tano katika karama hizo, ya kwanza ni wamishenari ama mitume. Neno *mtume* linamaanisha “mtu aliyetumwa,” neno *mmishenari* linamaanisha “mtu aliyetumwa.” Mmishenari anatumwa, na mtume anatumwa; Mungu humtuma mmishenari Wake, Mungu humtuma mtume Wake.

³¹ Ya kwanza ni mitume, manabii, waalimu, wainjilisti, wachungaji, hizo karama tano zilizotolewa na Mungu Kanisani. Kwa hiyo kila mmoja wenu ninyi watu aliye na mchungaji mtauwa, ana karama kutoka kwa Mungu kanisani mwenu, mchungaji, *mchungaji* maana yake ni “mchungu kondoo,” kulichunga kundi, kuwafundisha Neno la Mungu.

³² Halafu hizi karama zingine tisa mbalimbali za kiroho zinapaswa kuwa zikifanya kazi Kanisani kulidumisha Kanisa safi. Kama vile Anania na Safira, na kadhalika, Roho wa Mungu anainuka na kumwita mtu fulani, na kuwaambia wanaishi vibaya, na—na kukemea dhambi hiyo hadharani, na hiyo ndiyo sababu ya Roho Mtakatifu kuwa Kanisani, kulidumisha Kanisa safi na tayari kwa ajili ya kuja kwa Bwana, tunaamini hilo.

³³ Sasa, halafu kuna karama hizi zingine zinazolingia Kanisani. Sasa, baada ya mchungaji, basi mwinjilisti anaingia, halafu kuna waalimu wanaoingia, halafu kuna manabii wanaoingia, halafu kuna mitume wanaoingia, hawa wote pamoja, wakifanya kazi pamoja na karama, kulidumisha Kanisa katika ukamilifu, na safi, na tayari kwa ajili ya kuja kwa Bwana.

³⁴ Na kama wakati fulani huu wa kanisa ukilala mauti, ukimngojea Bwana, wakati wa pili wa kanisa unalala, hata kufikia zamu ya saba, haidhuru ni nyakati ngapi zitakazolala mauti, zote zitafufuka katika kule kuja kwa Bwana, na watanyakuliwa pamoja na hao walio hai na waliosalia ili kumlaki Bwana hewani. Nasi tunaitazamia Siku hiyo tukufu, nami ninaamini ya kwamba kama Mungu atatusaidia, kabla ya juma hili kwisha na—naamini ya kwamba tutaona vizuri zaidi kuliko hapo awali. Natumaini macho yangu yamefunguliwa kwa mambo mengi sana, pia, maana niko hapa kujifunza, kama sisi sote tulivyo.

³⁵ Niko hapa kuchota kwenu enyi watu kitu fulani ambacho, kipate kunisaidia. Watu wengi wanafikiri kwamba mwinjilisti hahitaji usaidizi wowote, umekosea, anahitaji msaada zaidi kuliko kusanyiko lote linavyohitaji, kwa sababu amesimama kati ya adui na kusanyiko.

³⁶ Sasa, nikiwa mgeni kwenu, nilifikiri ningechukua na kuelezea mambo haya, ili mpate kujua, kwamba tunaweza kuanza na kufanya mkutano mkuu katika eneo hili hapa. Nami ninaamini na kumtumainia Mungu, ya kwamba baada ya ibada hii kwisha, kwamba kila kanisa kote katika eneo hilo

litajaa washiriki wapya, na, wameongoka na kuingizwa ndani. Ninatumaini ya kwamba kupitia hilo kutakuwako na uamsho wa mtindo wa kale utakaofagia bonde hili hapa, ambao utawafanya watu kutoka kote nchini kumiminika hapa, wakitafuta...

³⁷ Ninaona ninaporudi Marekani, watu wenye njaa, baada ya mikutano yote mikuu na kadhalika ambayo tumekuwa nayo kote nchini. Tume kuwa na watu mashuhuri wakilivuka taifa letu, Billy Graham, Oral Roberts, na wengi wa hao mashujaa wakuu wa imani, watu mashuhuri, marafiki zangu binafsi. Nami najua wao ni watu wazuri, waliojazwa na Roho wa Mungu na waalimu wazuri sana.

³⁸ Na mimi mwenyewe, zaidi sana mimi ni mtu asiye na elimu, sina elimu, ninasikitika kwa hilo. Sikupata elimu ninayopaswa kupata. Nililelewa katika familia maskini ya watoto kumi, nami nilikuwa ndiye mkubwa kuliko wote, ilinibidi kufanya kazi niipatie familia riziki. Lakini, kwa namna fulani, Mungu katika majaliwa Yake makuu yenye hekima, aliona inafaa, huko nyuma kabisa kabla sijajua lolote kulihusu, kuniwekea mahali padogo pamoja nanyi watu. Na kwa hilo ninataka kuhudumu kwa moyo wangu wote, ku—kuwa ndugu yenu.

³⁹ Nami nisingekuwa hapa, kwa vyovyote vile ulimwenguni, kusababisha utengano wo—wowote, ama ugomvi wowote kanisani, bali nimekuwa hapa kujaribu ku—kuondoa ugomvi, na kuuleta Mwili wa Kristo pamoja, na kutufanya tujue ya kwamba sisi sote ni ndugu, kwamba sote tuko pamoja.

⁴⁰ Basi nilipotoka kwenye kanisa langu la Kibaptisti ku—kuhudumu miongoni mwa Wapentekoste, ambao wanaamini Ujumbe ambao Malaika wa Bwana alikuwa ameniletea, ndipo nilikuta kwamba walikuwa wabaya kama Wabaptisti, walikuwa na madhehebu mengi mbalimbali ya hayo, nami nikaona ndugu mashuhuri na wazuri katika kila moja la hayo.

⁴¹ Kwa hiyo ni—nisingeweza kusema, usiku wa leo, kwamba mimi ni mfuasi wa Assemblies, ama Church of God, na hata hivyo mimi ni mfuasi wao, kwa sababu sijajiunga tu na safu zao, bali nilizaliwa katika safu zao kama ndugu, nilipompokea Roho Mtakatifu. Nami nimejaribu kusimama moja kwa moja katikati ya pengo, na kuambia pande zote mbili, “Msibishane, ndugu. Sisi ni ndugu, hebu tumpende Bwana, na tusonge mbele, na kuungana pamoja.”

⁴² Mimi ni Mkentaki kwa kuzaliwa, nanyi nyote mnajua nembo ya Kentucky ni nini, ama, kauli mbiu, ni mkono uliopishana, namna *hii*, “Pamoja tunasimama, tukigawanyika tutaanguka.” Kwa hiyo, hatutaki makanisa yagawanyike, tunataka kusimama pamoja. Ingawa kwamba huenda tusikubaliane mmoja na mwingine, namna hiyo, hayo ni mambo madogo—madogo tu ambayo ni ya kimsingi, hebu tuamini kanuni kuu: Yesu alikufa apate kutuokoa sisi sote, Yeye ametupa sisi sote kuzaliwa upya,

nasi tunangojea kuja Kwake, na kufurahia sifa za kifo Chake mpaka atakapokuja, hivyo tu. Tunafurahia uponyaji wa Kiungu, Uwepo wa Roho Mtakatifu.

⁴³ Na kama Yesu Kristo ni yeye yule. . . Mungu anisamehe kwa kutoa tamshi hilo la “*kama Yeye ni,*” la kukufuru kulisema, lakini Yeye *ni* yule yule jana, leo, na hata milele, kwa sababu Neno linasema Yeye ni yule yule. Basi kama Yeye ni yule yule, basi angetendaje kama angalikuwa hapa duniani leo hii? Angetenda tu kama alivyotenda jana, kama Yeye ni yule yule. Mnaamini hilo, ninyi nyote? Angefanya hivyo. Ndipo kama angetenda vivyo hivyo, basi angefanya kazi zile zile alizofanya jana. Mnaamini hilo?

⁴⁴ Sasa, Maandiko yanasema, Yesu alisema Mwenyewe katika Yohana Mtakatifu 14:7, “Yeye alisikiaye Neno Langu. . .” la, “Kazi nizifanyazo Mimi, kwamba, yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Na fa—tafsiri ya Kiingereza hapo inasema, “*Kubwa kuliko* hizi atafanya, kwa kuwa naenda kwa Baba Yangu.” Lakini kama utachukua tafsiri ya asili juu ya hilo lililosema, “*Nyingi zaidi* atafanya.”

⁴⁵ Sasa, hakuna mtu angaliweza kufanya makubwa kuliko Yeye aliyofanya, kwa sababu Yeye aliwafufua wafu, akasimamisha maumbile, na kufanya tu kila kitu. Lakini jambo ni kwamba, kwamba, Yeye alisema, “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena,” sasa, neno hilo ni “Kosmos,” ambalo linamaanisha *utaratibu wa ulimwengu*, “hawataniona tena, bali ninyi,” Kanisa, “mtaniona, kwa kuwa Mimi,” na *mimi* ni kiwakilishi nafsi, tunajua hilo, “Nitakuwa pamoja nanyi,” Yeye hata amesema, “ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.”

⁴⁶ Sasa, ilikuwa ni nini basi? Mungu angeweza kujidhihirisha Mwenyewe kupitia Mtu mmoja, Mwanadamu, Mwanawe, aliyeitwa Yesu. Sasa, Mungu huchukua Roho ya Yesu huyo na kumrudisha ndani ya watoto Wake ambao wamefanywa wana wenye mamlaka na Yesu Kristo, na kudhihirisha Roho yule yule na nguvu zile zile, kote ulimwenguni. Huyo ni Mungu ndani yetu, Imanueli ndani yetu.

⁴⁷ Tumetakaswa kwa Damu ya Yesu. Nami ninaamini katika dini safi, kabisa, ya Roho Mtakatifu na utakatifu. Ninaamini ya kwamba mtu aliyesafishwa kutokana na maisha ya dhambi, huacha ulevi wake wote, kusema uongo, kuiba, na chochote kile. Ninaamini anamwishia Mungu, kwa sababu Roho aliye ndani yake ni Roho wa Mungu. Naye Roho huyo humwongoza na kumwelekeza katika haki na utakatifu, hata Mungu angeweza kuishi ndani yake, na kufanya ninii Yake, kufanya mapenzi Yake ndani yake.

⁴⁸ Sasa, kungekuwa na tofauti moja tu, basi, ingemzuia Yesu kuwa yeye yule aliyetembea Galilaya, kuwa hapa pamoja nasi usiku wa leo, ndani ya kila mmoja wetu. . . Sasa kumbukeni,

Yesu yule ninayenena habari zake ni Nafsi ya tatu, ambaye ni, Roho Mtakatifu, aliye ndani yetu, Mungu ndani yetu.

⁴⁹ Wakati Mwana wa Mungu... Mungu wakati mmoja aliishi katika Nguzo ya Moto, akawaongoza wana wa Israeli, ndipo akashuka na kuishi katika Mwanadamu, Mwanawe Mwenyewe, mwili ulioubwa, ndipo Yeye—ndipo Yeye akawa, akaja karibu zaidi nasi, basi ilimbidi autoe dhabihu mwili huo apate kuivunja ile Seli ya Damu iliyozaliwa na bikira, kulisafisha Kanisa apate kuishi katika moyo wa kila mtu ambaye angekubali Damu hiyo kwa ajili ya utakaso, Paulo anasema, ili kwamba aweze kuingia moyoni mwao kwa Roho Mtakatifu. Basi huyo ni Mungu akitenda kazi ndani yetu.

⁵⁰ Sasa, mwili halisi wa Yesu hauwezi kuwa hapa usiku wa leo. Huenda ukaja. Ingekuwa ni saa nzuri sana, sivyo? Kama mwili halisi wa Bwana Yesu, ambao umeketi mkono wa kuume wa Mungu usiku wa leo, kama ungeshuka kutoka Mbinguni uje duniani, tusingehitaji ibada zingine za uponyaji wala ibada za mahubiri, yote yangekwisha, Kule. Utakuja lini? Sijui, siamini mtu yeyote anajua, maana Yesu alisema hawakujua. Lakini Yeye alisema wakati alipoona ishara kama hizi tunazoziona siku hizi, tunajua ya kwamba wakati ulikuwa umekaribia.

⁵¹ Sasa, Yeye aliahidi mambo ambayo angefanya... ambayo nitayaendea baadaye katika jumbe. Lile wazo usiku wa leo juu ya kujiandaa, kwa namna fulani kufahamiana tu na kusanyiko. Tuna siku kumi usiku, na mara nyingi watu, usiponinii... kama ukikimbilia jambo fulani, bila kujua unalofanya, basi jambo la kwanza unalofanya, unajikuta umechanganyikiwa kabisa. Lakini kama ukiingia mstarini, unajua cha kutarajia hasa, ndipo unajua jinsi ya kupokea uponyaji wako. Jinsi ambavyo mara nyingi watu, katika kushughulika na kansa, uvimbe, ama kivimbe fulani, kiwe cha kufisha, ama si cha kufisha, mara nyingi wanashindwa kupata uponyaji wao wakiisha kuupokea mara moja.

⁵² Sasa, kivimbe ni kuzaliana kwa seli; hicho ni kitu kile kile ulicho wewe, kuzaliana kwa seli. Unajua mahali maisha yako yalikotoka, kwa sababu ilikuwa ni kwa njia ya ndoa takatifu. Nasi tunatambua ya kwamba mwanamke hana himoglobini, inatoka kwa mwanamume, na—naye mwanamume hutoa seli ya damu.

⁵³ Sasa, wengi wenu ninyi watu ni wakulima, nanyi mna kuku, mnao, angalieni uani mwone ndege, na ndege, mama ndege anaweza kujenga kiota chake na kutaga akakijaza mayai, naye anaweza kuyalalia hayo mayai na kuyashughulikia vizuri tu awezavyo kuyafanyia, na kujinyima chakula mpaka adhoofike sana, ni vigumu kwake kutoka kwenye kiota, akiyapindua mayai hayo, kwa uchaji, kila dakika chache, yapate kuanguliwa, akiyapasha joto, akijinyima chakula chote, na kadhalika,

ambacho angehitaji ili kuujenga mwili wake mwenyewe, yeye ni mwaminifu kwa mayai hayo, lakini endapo huyo mama ndege hajakutana na dume, hayo mayai kamwe hayataanguliwa, yataoza mumo humo kwenye kiota.

⁵⁴ Kuku, kuku wako wanaweza kutaga yai, kuku anaweza, anaweza kuyaatamia vivyo hivyo, wala kamwe halitaanguliwa, isipokuwa amekuwa pamoja na jogoo.

⁵⁵ Sasa, hivyo ndivyo ninavyowazia kuhusu kanisa siku hizi. Mnaona? Haijalishi tuna wafuasi wangapi, jinsi inavyotubidi kuwabembeleza na kuwaengaenga, kama hawajakuwa na Mwenzi, Yesu Kristo, na wamezaliwa mara ya pili, kamwe hawawezi kuamini uponyaji wa Kiungu, ama chochote kingine, una kiota tu kilichojaa mayai yaliyooza, ni bora kusafisha kiota na kuanza tena. Hiyo ni... Kama—kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo wanahitaji kusafisha kiota, uko Marekani, sasa hivi. Hiyo ni kweli. Tumewaingiza watu wengi kwa makosa, na kuwaweka kwenye kitabu cha kanisa, na kadhalika, ambalo ni sawa, afadhali wawe kanisani kuliko kuwa huko nje mtaani, lakini hata hivyo, tunachohitaji ni uamsho. Sasa, uamsho sio sana sana kuleta washiriki wapya, bali *kuwaamsha* wale ambao tayari wameingia. Mnaona?

⁵⁶ Ni kama tu bahari ye—yenu hapa. Niliketi kule karibu na ufuko hivi majuzi, walinipeleka kuvua samaki jana, baada ya kuwa na mapumziko ya siku moja, nami nikaangalia bahari hiyo kuu, yenye nguvu, ikiyavuruga mawimbi hayo juu chini. Nikawaza, “Kwa nini imefadhaika hivyo? Kwa nini inayavuruga mawimbi?” Nikawazia, “Hakuna hata tone moja la maji zaidi ndani yake, kuliko ilivyo wakati ni shwari kabisa.” Hiyo ni kweli. “Mna kiasi kile kile cha maji, hamna maji zaidi hata kidogo, lakini vurugu hiyo ni ya nini?” Nikawaza, “Ina uamsho.” Inafanya nini? Inatikisa hizo takataka zote kutoka majini, hadi ukingoni.

⁵⁷ Kwa hiyo, huo ndio—huo ndio kanisa linahitaji leo ni uamsho, kutikisa kutokuamini kwote kutoka kwetu, mpaka tuweze kuwa safi. Hivi hamwoni hivyo? Kwa yote... Ninachomaanisha na *dhambi* ni “kutokuamini.” Tunatambua ya kwamba hiyo ndiyo dhambi pekee iliyopo, ni kutokuamini, tunaamini ya kwamba, “Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa tayari.”

⁵⁸ Kama nilivyosema wakati mmoja, wakati fulani uliopita, nikihubiri katika kanisa la Kimethodisti, nilisema, “Kuvuta sigara, kunywa wiski, kufanya uzinzi, kusema uongo, kuiba, hiyo si dhambi.”

⁵⁹ Ndipo maskini dada mpendwa wa thamani aliyeketi pale, amevaa moja ya maskini ukosi uliopinduliwa, aliyefundisha utakatifu maishani mwake mwote, akasema, “Naomba uniambie, dhambi ni nini?”

Nilimkaribia tu, nikasema, “Dhambi ni kutokuamini.”

⁶⁰ U—unafanya mambo hayo kwa sababu huamini. Yeye amwaminiye Bwana asingefanya mambo hayo, amepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Yesu alisema katika Yohana Mtakatifu 5:24, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele,” kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na huo ni Roho Mtakatifu, mnaona, “yeye yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita,” wakati uliopita, “amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Loo, napenda hilo, nanyi je? “Yeye aaminiye.”

⁶¹ Sasa, sisi... Daima mkutano hutoa matabaka matatu ya watu, asiyeamini, anayejifanya mwaminio, na mwaminio. Tulikuwa na hilo katika... Sikuzote tumekuwa nalo, na tu—tutakuwa nalo daima. Na kwa hiyo, tunataka kumfanya a—asiyeamini awe mwaminio, na anayejifanya mwaminio awe mwaminio halisi. Kwa nini tukubali kabadala wakati mbingu zimejaa yaliyo halisi? Kwa nini tunataka kitu ambacho ni cha kubuniwa sana, na loo, kitu fulani, lundo la mhemuko, ama chochote kile?

⁶² Sasa kumbukeni, ninaamini ya kwamba Roho Mtakatifu ana mhemuko mwingi. Chochote, ninaweza kukuthibitishia chochote ambacho si, kisicho na uhai ndani yake kimekufa. Kwa hiyo kama kanisa halina uhai mdogo, hilo kanisa lina kasoro, linahitaji ufufuo. Kwa hiyo ninaamini inatubidi kuwa na mhemuko. Tunapata...

⁶³ Ninaona tuko kwenye sakafu ya mpira wa vikapu. Sasa, wengi wenu ninyi watu, watoto hapa, mnaenda shuleni. Hakika ninamshukuru Mungu kwa ajili ya shule hii nzuri, ndiyo shule nzuri kuliko zote niliyopata kuingia, ninaamini, kwenye kumbi za mikutano, nimekuwa katika nyingi. Lakini mimi... hapa... Vipi kama ulikuwa na mchezo wa mpira wa vikapu hapa, na timu yako ilikuwa ikishinda, loo, jamani, umeketi tu pale kwenye roshani? Ungesema, “Ndio mchezo mbaya sana, niliowahi kuhudhuria.” Mbona, hakika.

⁶⁴ Vema, kama Bwana wetu anashinda vita, nawaambia, hi—hi—hiyo, hakika tungeweza kukatakata kidogo mara moja moja, mwajua, kumfahamisha ya kwamba tu—tunathamini ushindi ambao Yeye ametupa. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, hatutaki iwe ni mkutano uliokufa, kanisa lililokufa, tunalitaka likiwa hai, huku Roho wa Mungu akitenda kazi, katika Injili halisi, ya busara, na akili timamu, akifanya tu ishara kuu na maajabu, na kuonyesha ishara za Masihi miongoni mwetu.

⁶⁵ Wakati Israeli waliposafiri kutoka, kutoka Misri hadi kwenye nchi ya ahadi, walipokuwa safarini mwao Balaamu hakujua ya kwamba kulikuwako na Sauti ya Mfalme kambini. Alisahau kuona ule Mwamba uliopigwa na yule nyoka wa shaba, na sha—shangwe ya ushindi wa Mfalme.

⁶⁶ Hilo ndilo tunalotaka usiku wa leo, tuna Mwamba uliopigwa kambini. Mnaamini hilo? Huyu ndiye Mwamba, Kristo Yesu. Alipigwa kama ule Mwamba ulivyopigwa nyikani, na fimbo ya hukumu ya Mungu, Naye akabeba hukumu zetu, hivi kwamba kama vile hao watu waliokuwa wakiangamia walivyopata nguvu tena, na kupewa uhai mpya kutokana na yale maji yatokayo Mwambani, vivyo hivyo na Kanisa, kila linaposema na ule Mwamba, linapata maji mapya yanayobubujika, Uhai mpya, na kuamshwa tena.

⁶⁷ Halafu Yeye alikuwa na nyoka wa shaba akifanya upatanisho kwa ajili ya dhambi zao zote walizotenda, maji ya farakano yaliyofanywa nje ya kambi kumtenganisha asiyeamini na kutokuamini kwake. Walikuwa na hayo yote, halafu katikati ya hayo yote, kulikuwa na shangwe za ushindi wa Mfalme kambini wakati wote. Kwa hiyo, tuko kwenye safari yetu usiku wa leo, na hebu tumtumikie Bwana kwa moyo wetu wote.

⁶⁸ Sasa, tutajaribu kila usiku kuwaachilia... Sisi, nafikiri tulianza usiku wa leo kwenye saa mbili na nusu, na labda kesho usiku tutaanza mapema kidogo. Halafu kesho usiku ninataka kuingilia somo zaidi pamoja nanyi juu ya uponyaji wa Kiungu, ili mpate kufahamu kabisa.

⁶⁹ Jambo moja dogo ninalotaka kuingiza mumu humu, ambapo kama nikilisahau kesho usiku, hebu tuchukue kwa mfano, ki—kivimbe, uvimbe, kansa, chochote kile. Kilianzaje? Kama vile mkono wangu hapa, hakuna kitu mkononi mwangu sasa, siku moja huenda kukawa na kivimbe, kansa, chochote kile, uvimbe. Uvimbe huo ni nini? Ni mahali fulani ambapo kuna chembechembe nyingine ndogo inayoingia mle na kuanza kufanya seli, na ni kuzalisha seli. Kama tu vile wewe ulivyoanza katika tumbo la uzazi la mama, ukaanza kukua ukawa mwanadamu; mbwa anakuwa mbwa, kuku anakuwa kuku, na kadhalika.

⁷⁰ Lakini uvimbe, kansa, ama chochote cha vivimbe hivyo, havina umbo lolote maalum, kwa sababu vina... havikuumbwa kwa mfano wowote wa mwanadamu. Baadhi yake vina miguu, na baadhi yake ni mviringo kama chapati, na vingine vya mstatili zaidi. Ni kitu gani? Ni pepo. Yesu aliviita pepo. Je, alikuwa sahihi? Bila shaka, alikuwa sahihi. Kwa sababu neno *ibilisi*, linamaanisha “mtesi,” kansa, uvimbe, na magonjwa yanayokutesa.

⁷¹ Sasa, agizo la mwisho Yesu alilolipa Kanisa Lake lilikuwa, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini, atahukumwiwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, kwa Jina Langu watatoa pepo.” Mnaamini hilo? “Kutoa pepo.”

⁷² Basi inakuwaje kama uhai uliacha uvimbe huo? Tutauita uvimbe ama kansa, ndio mwuaji mkuu kuliko wote. Sasa, kama

uhai ukiiacha hiyo kansa, mara moja, inakuwaje uhai huo ukikuacha? Kwa siku ya kwanza au karibu hivyo, mwili wako husinyaa.

⁷³ Kuna wawindaji wangapi hapa ndani, wanaowinda kulungu na wanyama? Vema. Sasa, ukimwua kulungu leo, nawe useme, ama bucha, ama chochote unachotaka kuwa, hata mtayarisha mazishi, unaona, useme, “Mwili huu,” uweke kwenye mizani, “una uzito wa ratili mia mbili na hamsini,” kuwa mwangalifu yale unayowaambia hao wavulana, sasa, unapoupima asubuhi, utakuwa mwepesi kwa ratili kadhaa. Unajua hilo, sivyo? Utapungua kwa asilimia kubwa usiku mmoja. Mwili wa mwanadamu hufanya vivyo hivyo, mwili wowote wa seli hufanya vivyo hivyo, kwa sababu unakauka.

⁷⁴ Sasa, basi acha ukae hapo kwa muda wa siku tatu ama nne tu kwenye jua, kisha uuchukue; hebu maskini mbwa akanyagwe barabarani, na umwache alale hapo siku tatu ama nne katika jua hilo kali, angalia kinachotukia. Atakuwa karibu mara mbili ya ukubwa wake, ndipo yeye ni mzito kuliko alivyowahi kuwa.

⁷⁵ Sasa, kama mwanadamu, wakati roho hii...Mnaona, hatushughulikii kivimbe hicho, hicho ndicho daktari anachoshughulikia, daktari hushughulikia kile anachoweza kugusa, ama kile anachoweza kuona. Hisi zake mbili kati ya tano anazoweza kufanya kazi nazo, hizo ni kugusa kwake ama kuona kwake. Sasa, anagusa hicho kivimbe, anakifanyia upasuaji, anakiangalia, anakitoa, sasa, kama kuna kipande cha mzizi kilichosalia, kinaendelea tu kukua. Mnaona?

⁷⁶ Sasa, hatushughulikii kivimbe hicho hata kidogo katika uponyaji wa Kiungu, tunashughulika na uhai ulio katika kivimbe hicho, ibilisi mwenyewe, uhai huo. Ndipo wakati uhai huo unapotoka, mara moja, ama saa chache, huyo mgonjwa anaanza kupata nafuu, anajisikia vizuri, anaenda akishuhudia. Kwa kawaida baada ya siku tatu ama nne, mimi nimeondoka mjini. Mnaona?

⁷⁷ Vema basi, Biblia inasema, “Kwamba pepo mchafu anapomtoka mtu, hutembea mahali pasipo na maji. Anarudi na pepo saba wabaya kuliko alivyokuwa, na iwapo mwenye nyumba hayuko pale kulinda, pepo huyo ataingia moja kwa moja tena, na hali ya mwisho ya mtu huyo ingekuwa mara nane ya ilivyokuwa hapo mwanzo.” Mnaona? Angekuwa na vitu vingine saba mbalimbali. Sasa, hatuna budi kuamini hilo, maana Mungu alisema hivyo, na hilo ni Neno Lake. Inatubidi tu kuushughulikia ujumbe wetu kutokana na hilo, mnaona, ya kwamba Hilo ni kweli, kwa sababu ni Neno la Mungu.

⁷⁸ Sasa, kama watu wakiingia moja kwa moja ndani, labda wakiwa na mkutano wa siku tatu usiku, watu waingie mumo humo ndani, waombewe, “Loo, nimeponywa, najisikia vizuri zaidi,” atoke kwenye kitanda cha wagonjwa, aende nyumbani,

yapata saa tisa ama kumi, yapata saa sabini na mbili, uharibifu unaingia, na uozo unaanza kuvimba, kisha kasema, “Loo, nilipoteza uponyaji wangu! Loo, ni—nilipoteza uponyaji wangu!” Hiyo ndiyo ishara iliyo bora kuliko zote ulimwenguni, umepata uponyaji wako. Unaona? Hiyo ndiyo ishara umeupata, hujaupoteza.

⁷⁹ Na mambo madogo rahisi kama hayo, ambayo kanisa linapaswa kufundishwa. Mnaona? Kujua jinsi ya kushikilia. Usiruhusu kutokuamini kuingie, mara unaposema, “Loo, nimeupoteza,” upesi hivyo, Shetani anarudi tena. Hiyo ni kweli. Basi uko hali mbaya kuliko ulivyowahi kuwa. Unaona?

⁸⁰ Na hiyo ndiyo sababu mikutano yangu haijawahi kuwa na wakati wa kutosha ambapo ningeweza kulielezea, na kuingia miongoni mwa watu na kuwaambia habari zake. Basi baadhi ya siku hizi, Bwana akipenda, nitachukua hema kubwa na kuhamia mahali fulani ambapo ningeweza kukaa majuma matatu ama manne kwa wakati mmoja, ama matano, kuendelea tu, niache mgonjwa huyo arudi tena, na kuwathibitishia, na kuwaonyesha ya kwamba kitu hicho kimekwisha, maana Mungu hana upendeleo. Yeye atakayemponya mtu mmoja aliye na kansa atamponya mtu huyo mwingine aliye na kansa, kama akija katika msimamo ule ule, kwa msingi ule ule.

⁸¹ Kwa sababu, waweza kuwachukua watoto wako, ukaketi mezani, na kila mmoja wao ana njaa, na kusema, “Sasa, unaweza kunywa bilauri ya maziwa, usije ukafa, lakini wewe, John, huwezi kuinywa, Joe anaweza kuinywa”? Usingefanya hivyo. Unampenda John kadiri unavyompenda Joe, kama ninyi ni wazazi wa kweli. Vema, kama unajua jinsi ya kufanya mema, kuwapa watoto wako vipawa vyema, si zaidi sana Baba yenu wa Mbinguni anajua kuwapa watoto Wake vipawa vyema? Kwa hiyo, mnaona, kila mmoja wetu anaweza kuponywa.

⁸² Nami nimeona mengi sana yakifanywa, nawaambia, enyi marafiki, mpaka mimi, ninajua tu Mungu anaweza kufanya kila kitu. Nimeona ukoma katika hatua yake ya mwisho, ukiponywa. Nimeona watu waliokuwa, nina taarifa za madaktari za watu waliokuwa wamelala wakiwa maiti, wakachunguzwa na madaktari, wamekufa, wakafufuka tena, kwa imani, kuamini tu. Mnaona?

⁸³ Na maskini mama mmoja akisimama juu ya mtoto wake mchanga, na kumwona mtoto huyo akifufuka baada ya kuwa, amekufa asubuhi hiyo saa tatu, na hii ilikuwa karibu saa nne na nusu usiku huo, hivi majuzi tu, huko chini Meksiko. Nikasema, “Usitangaze hilo, acha daktari atie hiyo sahihi.” Mnaona? Kwa hiyo, tunapotoa tamshi, halina budi kuungwa mkono, mnaona, kwamba ni kweli.

⁸⁴ Hatuiachi itangazwe, kwa sababu, huko nje, mnajua ninalomaanisha, mambo makubwa, kwa sababu ninii, mnajua,

sisi Wamarekani tunatazamia mambo *makubwa*, mambo *makuu*, kelele nyingi kwake, mnaona, loo, Hollywood nyingi. Mungu na atusaidie tuyaondokee hayo, tuirudie Injili. Hiyo ni kweli. Nimechoka sana na kudhoofishwa na uinjilisti wa Hollywood, na kuona mamilioni wakifa huko nje bila kumjua Kristo hata kidogo. Mnaona? Hakika inaudhi. Jinsi hilo lilivyo kinyume na Mungu!

⁸⁵ Eliya, ule upepo ukienda kasi haukumvutia, zile kelele za ngurumo hazikumvutia, tetemeko la nchi halikumvutia, lakini aliposikia Sauti ndogo tulivu, ndipo huyo nabii akaufunika uso wake na kutoka nje. Hilo ndilo lililouvutia usikivu wake. Basi ndugu, dada, hebu tusikilize juma hili ile Sauti ndogo tulivu, mnaona.

Sasa, kabla hatujalikaribia Neno Lake, kulisoma, hebu na tuinamishe kichwa chetu kwa muda kidogo tu, kuomba.

⁸⁶ Sasa, Baba Mungu, tunalikaribia Neno Lako katika Jina la Bwana Yesu, kwa sababu kwamba Wewe uliahidi kama tukiomba lolote katika Jina Lake, tungelipokea. Nasi tuna hakika ya kwamba Neno Lako ni kweli, kwa sababu tumekuja kwenye mji huu mdogo wenye neema, ambao umetualika hapa, na hawa watumishi Wako wote wazuri, waliokusanyika hapa, na hawa ndugu wahudumu wa thamani hapa nyuma, nyuma yangu kuomba, wakilinda kundi lao, hapa nje, wachungaji waaminifu. Jinsi ninavyokushukuru kwa ajili ya jambo hilo, Baba!

⁸⁷ Na kondoo wengi wagonjwa wanangojea ile saa upate kuwakomboa. Hawawezi kuendelea mbele zaidi, Bwana, daktari amewalaza wengi wao nyuma, labda, kwamba moyo wao ni mbaya sana hauwezi kufanya kazi tena, kansa itawaua, naye daktari amefanya yote ajuayo kufanya. Tunashukuru kwa ajili yake, na maarifa ambayo Wewe umempa.

⁸⁸ Lakini sasa, Baba, bado kuna hatua nyingine tunayoweza kupiga, na hiyo ndiyo sababu tuko hapa. Baadhi yao wako hapa wakiwa na nafsi zilizo na ugonjwa wa dhambi, hawajui furaha ya kukutumikia Wewe, Bwana, na kukujua Wewe kama Rafiki binafsi anayetembea nawe barabarani, anayesafiri pamoja nawe kwenye gari, anayezungumza nawe katika chumba cha siri, anayekula pamoja nawe mezani. Ee Mungu, jalia Yesu awe Rafiki binafsi, Mtu mmoja tu wa familia katika kila nyumba iliyo hapa katika jiji hili, kote katika eneo hili. Tujalie, Bwana.

⁸⁹ Tunaomba sasa ya kwamba utabariki jitihada zetu dhaifu tunapojaribu kuweka, mbele ya marafiki zetu wa thamani, Injili. Na, Bwana, utanisaidia? Mimi ndiye ninayehitaji usaidizi. Na kama ningesema jambo lolote, ama kujaribu kusema jambo lolote ambalo lilikuwa kinyume na mapenzi Yako au Neno, basi, Baba, Wewe ungali ni Mungu yeye yule ambaye angeweza kufunga kinywa cha simba katika lile tundu pamoja na Danieli, angeweza kufunga langu, pia. Nami naomba ya kwamba Wewe

hutaniruhusu niseme jambo moja, ila lile litakalokuwa la kulijenga, na kwa, kwa Kanisa Lako na kwa watu Wako.

⁹⁰ Pia jalia kila mgonjwa aponywe, jalia kila mtu aliyepotea aoko, kila aliyerudi nyuma arudishwe kwenye ushirika tena. Libariki Neno Lako tunapolisoma usiku wa leo kwa ajili ya somo hili dogo, jalia liweke matayarisho pamoja kwa ajili ya wa—wakati halisi katika siku hizi chache usiku zinazofuata katika ibada Yako. Na ibada zitakapofungwa, basi tutainamisha vichwa vyetu na mioyo yetu kwa unyenyekevu mbele Zako, na kukupa Wewe sifa zote na utukufu. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Mwanao mwema na mpendwa, Bwana Yesu Kristo, Mwokozi wetu. Amina.

⁹¹ Sasa, kwenu ninyi ambao, kwa kawaida mnaweka somo, ama maelezo ya somo, ama mahali, ninawatakeni mfungue usiku wa leo katika Yohana wa Kwanza, mlango wa 5, na kifungu cha 4, kusoma tu maneno machache; ninataka fungu dogo kutoa muktadha.

⁹² Na wakati mkifungua, huenda nikasema kwamba sasa jioni tunazowaomba wagonjwa, ili kudumisha utaratibu, hao wavulana watakuwa hapa chini yapata saa moja kabla ya ibada kuanza, wakigawa kadi za maombi kwa mtu yeyote anayezitaka. Wanachukua kadi za maombi na kuzileta mbele za watu, wanachanganya kadi hizo zote za maombi, wanazileta huku chini na kumpa mtu yeyote anayezitaka, nazo hizo kadi za maombi zitatumiwa usiku huo.

⁹³ Usi—usizilete, au kumpa mtu mwingine yeyote, wewe—wewe ambaye umesikia maagizo, wewe ndiwe unayepata hiyo kadi ya maombi. Basi kama una rafiki fulani anayetaka kadi ya maombi, basi acha waje hapa wasikie maagizo ambayo Bw. Borders, na hao wengine watakuwa wakiwapa, maagizo, wahudumu, na kadhalika. Nazo kadi za maombi hazibadilishanwi, zinapaswa kupewa kila mmoja.

⁹⁴ Na ndipo wataita kwa namba kuja jukwaani. Basi, hilo linalifanya hivi kwamba hakuna mtu anayejua ambapo mstari wa maombi utaanzia, hakuna mtu anayejua ni kadi zipi.

Wasema, “Nipe kadi ya maombi namba moja.”

Vema, kama ulikuwa na namba moja, huenda tukaanzia kumi na tano.

⁹⁵ Kwa sababu nilijaribu hili, tulijaribu bila kadi za maombi, nena kuhusu msukumano! Kwa kweli huu ungekuwa uwanja wa michezo. Halafu basi, tuna ninii... Kisha tulijaribu hilo. Halafu nikajaribu kutuma kadi za maombi mia moja kwa kila mchungaji tunayeshirikiana. Ndipo basi mchungaji wa kwanza akaingiza kundi lake, hao wengine hawakuwaingiza wakati mkutano ulipokuwa ukiendelea, maana wakati tulipowamaliza hao, na hiyo mistari inayosonga polepole, kwa sababu hatuwaruhusu wapite mpaka tutakapokuwa na hakika kila

kitu ni sawa. Kwa hiyo, nafikiri hivyo ndivyo mnetaka. Hiyo ni kweli?

⁹⁶ Halafu basi—halafu basi, mara nyingi kuna hamsini walioponywa katika, huko nje, wakati kuna mmoja aliyeponywa jukwaani, kwa hiyo haijalishi sana kuhusu hilo. Naye Roho Mtakatifu huenda moja kwa moja kwenye kusanyiko, kama tutakavyolifikia mbele zaidi, Yeye huponya vivyo hivyo tu.

⁹⁷ Lakini zile kadi, ndipo mnaona, basi kile tulichofanya, tusingeweza kufanya hivyo, maana mchungaji wa kwanza aliyeingiza watu wake, yapata kadi mia moja, kwa ajili ya mkutano wa siku tatu usiku, hilo lilitosha.

⁹⁸ Na halafu lingine tulilofanya basi, ningeshuka niende nikagawe kadi za maombi, nami ningekuja, ningesema, “Hebu, kama mvulana huyu mdogo, hapa, na aje ahesabu, na mahali atakaposimamia, tutaanzia hapo.” Amini usiamini, mama alimfanya kadogoo asimame papo hapo kwenye kadi yake, mwajua. Kwa hiyo, sisi tungali ni wanadamu, tunatambua hilo, na tulipata malalamiko juu ya hilo.

⁹⁹ Halafu nilikuwa na jamaa mmoja aliyekamatwa katika mikutano yangu akiuza hizo kadi za maombi, akimhakikishia mtu fulani kwamba wangeingia kwenye mstari wa maombi, usiku mmoja ulimmaliza mtu hivyo.

¹⁰⁰ Kwa hiyo, nikamwagiza mwanangu mwenyewe kusambaza kadi za maombi, nami ninajua kwamba hatakuwa na hiyo. Halafu basi, nikapanga kwamba watu wasingejua ambapo mstari wa maombi ungeanzia, yeye huleta kadi za maombi mbele za watu na kuzichanganya zote, kisha anawapatia tu papo hapo, popote mzitakapo, kwa hiyo yeye mwenyewe hajui, hakuna mtu mwingine anayejua.

¹⁰¹ Ndipo basi—basi ninapokuja mkutanoni, ninaliacha tu popote Roho Mtakatifu, nimefanya mara nyingi, kuhesabu ni wangapi katika safu *hii*, na kuondoa safu *hii* kutoka kwake, kuigawanya kwa safu *hiyo*, na kadhalika namna hiyo, ama popote tu Roho Mtakatifu angeniongoza kuanzia, hapo ndipo tunapoanzia. Halafu sisi, kabla ya ibada kumalizika hata hivyo, sikuzote tunamwombea kila mtu anayekuja mkutanoni, daima tunapata hiyo.

¹⁰² Halafu, tunataka kuwajulisha, pia, hatujaribu kusema, “Sasa, mwinjilisti yuko hapa, yeye ndiye atakayeponya.” Tunawajulisha ya kwamba mchungaji wenu ni mtu wa Mungu, mwenye mamlaka yale yale ya kuwaombea wagonjwa, kama mimi, ama mtu mwingine yeyote, mimi, Oral Roberts, ama Tommy Osborn, ama yeyote—yeyote wa watu walioko hudumani siku hizi, wakiwaombea wagonjwa, mchungaji wako ana mamlaka yale yale. Huenda asihudumu chini ya karama ile ile, lakini angali ni mtumishi wa Mungu, akihudumu chini ya

karama aliyopewa na Mungu. Kwa hiyo, sikuzote tunakumbuka hilo.

¹⁰³ Na sasa, mnakuja yapata . . . Mimi . . . Utaanzisha ibada saa ngapi, Ndugu, kesho jioni? Saa moja na nusu. Basi mnapaswa kuwa hapa saa kumi na mbili u nusu, ili ninyi . . . hawataingilia mkutano uliosalia, waanze kugawa kadi mpaka wakati huo, kwa hiyo njoni mapema mwezavyo, ili zote hazitakuwa zimekwisha mtakapofika hapa. Ndipo kila usiku watakuwa wakigawa kadi ambazo tunawaomba wagonjwa, na hiyo hupunguza mkurupuko mkubwa, na kila mtu, na halafu wanapandana.

¹⁰⁴ Loo, jamani, mnapaswa kuona katika nchi za kigeni ambako sisi . . . karibu inakubidi kuchukua wanamgambo. Nimewaona wakikanyaga ku—kundi la askari watano mstarini, nikamwona mwanamke akiruka juu ya mabega ya wanaume, na kupita mbio moja kwa moja, akirukia mabega ya wanaume hao. Akivuruga safu yote ya jeshi, kitu kama hicho, akipitia katikati ya miguu yao, labda elfu nne ama tano ya hao kwa wakati mmoja wakikurupuka tu namna hiyo, na kupenya tu, kwa vyovyote vile, akuruarilie nguo, na kadhalika, akijaribu tu kukugusa, ama chochote kile. Kwa hiyo, tunao hapa, tunaweza kuwa na utaratibu katika mikutano midogo kama tuliyo nayo sasa, na kuifanya kwa heshima, na kwa mpangilio. Hivi huamini hilo?

¹⁰⁵ Vema sasa, tunaposoma mlango wa 5, na kifungu cha 4 cha Yohana wa Kwanza:

*Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu
huushinda ulimwengu: na huku ndiko kushinda
kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu.*

Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake.

¹⁰⁶ Sasa, ninataka kuzungumza usiku wa leo juu ya somo la *Kile Kinachohitajika Kukushinda Kutokuamini Kwote: Imani Yetu*.

¹⁰⁷ Sasa, tunafunga tu, jana, ambapo tulikuwa na kampeni mbili kuu hapa Marekani, moja ilikuwa ni ya Wanademokrasia, walikuwa na yao huko California, na magazeti yote yalikuwa yamejaa hayo, usingeweza kufungua redio bila kuisikia. Hiyo ni sawa, hicho ndicho chama. Nao wakamchagua yule waliyemdhania kuwa ndiye mtu bora zaidi kwa chama chao, nao wakamchagua Bw. Kennedy. Ndipo basi walipomchagua Bw. Kennedy katika mkutano wao, na, loo, walijenga jukwaa kwa ajili ya Bw. Kennedy kuwa mtu mashuhuri kuliko wote ulimwenguni leo. Ndipo basi, hatimaye walipomchagua mtu waliyetaka achaguliwe, wote walishangilia na kumsifu sana Bw. Kennedy.

¹⁰⁸ Na jana, ama, siku moja kabla, wakati wowote ule, wakati chama hicho kingine, chama cha Republican kilipomchagua Bw. Nixon, vema, walihubiri kwa siku kadhaa, wakimjengea jukwaa Bw. Nixon, na, kwenye kampeni yao. Nao, hatimaye,

wakati chama hicho kilipomchagua mtu ambaye walidhani walitaka agombee urais wa Marekani yetu tunayoipenda, umati ulifurahia, na kushangilia, na kupiga mayowe, na kuruka juu chini, kwa sababu walikuwa wamemchagua mtu ambaye walikuja katika kampeni hiyo kumchagua.

¹⁰⁹ Sasa, tumekuja hapa, usiku wa leo, kumchagua Mtu, na Mtu huyo ni Bwana Yesu. Nami ninajaribu kumjengea jukwaa usiku wa leo, ili kwamba katika siku zijazo usiku wa uamsho huu tupate kushangilia, na kulisifu Jina Lake, kwa sababu kwamba tumemchagua Yeye mioyoni mwetu kuwa Mwokozi wetu, Mungu wetu, Mponyaji wetu. Na kwanza, tunataka kumwekea jukwaa.

¹¹⁰ Na sasa, tutazungumza juu ya imani na ushindi. Na kumekuwa na ushindi mwingi mkuu uliopatikana katika ulimwengu huu. Hapo, kama ningeweza kuuhesabu usiku wa leo ungeingia katika maelfu mengi ya ule ushindi mkuu ambao umepatikana kote ulimwenguni, siku za kale za Rumi, na Uyunani, na kadhalika, na wale mashujaa wakuu ambao wamepata ushindi mkuu, mpaka dunia nzima imejaa damu ya wafia imani.

¹¹¹ Huenda nikawakumbusha wawili au watatu, ili tu waweze kuanza, na jinsi wanavyotenda wakati ushindi huo umepatikana. Kwa mfano, wakati Wa—Wajerumani katika vita vilivyopita, ama Vita vya Kwanza vya Dunia, vya Pili ilikuwa, waliopata ushindi huko Ufaransa, na baada ya kufanya kila kitu salama, walitengeneza jukwaa kwa ajili ya Hitler, naye Hitler akasimama pale, wakasema, kwenye ile Tao ya Ushindi. Mimi mwenyewe nimesimama pale mara nyingi. Na wakati aliposimama pale, kwamba makumi ya maelfu ya maelfu ya Wajerumani walipita kwa hatua za kwenda bila kukunja miguu, pamoja na saluti ya Kijerumani kwa Kiongozi wao aliyesimama kwenye jukwaa lake walilokuwa wamemjengea.

¹¹² Na inasemekana anga, kama wingu kwa nusu saa ya ndege zilizojengewa Ujerumani zikipita juu. Watu walipiga mayowe, bunduki zikapigwa, filimbi zikapigwa, kengele zikalia, kila kitu, kwa sababu walikuwa wamepata ushindi na walikuwa wameiteka Paris, wameiteka Ufaransa.

¹¹³ Na hapa siku moja, kwenye lile kongamano la ulimwengu, Kongamano la Kipentekoste Ulimwenguni, huko London, Uingereza, walikuwa wakionyesha sinema kule ya Stalin, walipomleta wakati Ujerumani ilipoanguka nao wakamleta Berlin. Na hiyo ilikuwa ni tamasha ya jinsi gani kuwaangalia hao Waje-... ama, vifarua vilivyojengwa na Warusi vyenye banda la mizinga vikiwa kidogo juu ya vichwa vya kimoja kwa kingine, vimelengwa kikamilifu kwa sababu mfyatuo mmoja mkali ulienda kote. Loo, sioni jinsi ulimwengu ungeweza kudumu chini ya mshtuko wa kutisha sana kama waliouelekeza Ujerumani. Jinsi ambavyo hizo bunduki zililengana zenyewe kidogo moja

juu ya nyingine, na ni mandhari tu, wakiendelea kufyatua kwa makombora hayo makubwa sana yaliyolipua mabonge ya marisau, waliirarua tu Ujerumani vipandevipande.

¹¹⁴ Na hatimaye walipojisalimisha, nao wakaingia ndani wakapafanya salama na kuleta jukwaa na kumleta Stalin kwenye ndege alipotua, ambapo, Warusi wakiwa na maskini kitu hicho cha kigeni, kilichoinama chini na juu, makumi ya maelfu mara maelfu ya askari wa Kirusi waliingia ndani wameinama, na huku na huko, huku wakishangilia, na kupiga mayowe, na kupaza sauti, na kupiga makelele, kwa sababu walikuwa wamepata ushindi dhidi ya Ujerumani, walikuwa wamewashinda kabisa.

¹¹⁵ Basi ilikuwa ni kitu kama hicho siku ile amani ilipotiwa sahihi wakati tulipokuwa tumerusha bomu la atomiki juu ya Hiroshima, na kuwalipua yapata watu milioni moja vipande-vipande, na kuliteketeza maskini genge lote mpaka matumbo yao na mboni za macho zikaanguka, na ndipo Japani ikajisalimisha.

¹¹⁶ Basi ilipofanya hivyo, filimbi zikalia, na bunduki zikafyatuliwa, na mayowe yakapigwa, na kila kitu, ndipo baba wengi wakafurahi kwamba vita vilikuwa vimekwisha, kwa sababu kwamba wangepata raha kidogo. Baba na mama wengi walifurahi, kwa sababu mwana wao angerudi nyumbani tena. Na ilikuwa ni—ilikuwa ni siku kuu. Na chochote kinachopata ushindi, ni kushinda kitu fulani, kinashinda kitu chao wanachopigania.

¹¹⁷ Nimesimama misituni huko Afrika Kusini wakati nikiwinda simba, na hapa yule simba ambaye nilikuwa nikidhani alikuwa ni mla mizoga mwenye upele, bali nilimheshimu, kwa sababu akiwa na nguvu zake zote kuu za kuua yeye huua tu apate kula. Wanyama wanaweza kumkanyaga siku nzima, akiisha kula, hatawajali.

¹¹⁸ Lakini anapoua kitu, ni jambo la kusikitisha kumwangalia. Atamwua ko—kongoni, ama punda milia, ama kitu fulani, ataweka miguu yake juu yake, kisha akitupe kichwa chake kikubwa hodari hewani, na nywele zenye matimutimu shingoni mwake, naye *atanguruma*.

¹¹⁹ Loo, nimesimama umbali wa yadi mia tano na kuona changarawe ndogo zikianguka ardhini, na kutoka kilimani na kulingirika chini, kutokana na mlio huo wa kutisha sana wa kilio hicho cha ushindi anachotoa. Alipata kitu cha kula, naye anaweka miguu yake juu yake, anakiramba, ananguruma msituni.

¹²⁰ Mambo haya yote hayadumu. Vita hivi na umwagikaji wa damu, vinarudi moja kwa moja tena, kwa sababu vimeshindwa kwa njia mbaya, hayawezi kudumu. Hakutakuwa na amani mpaka Yesu atakapokuja na kuweka Ufalme Wake, ndipo

ulimwengu hautasomea vita tena, lakini mpaka wakati huo mataifa yanatawaliwa na ibilisi, kama Biblia inavyosema, nayo yatapigana mpaka Yesu atakapokuja.

¹²¹ Jinsi ilivyokuwa siku hiyo, wakati Shetani alipompeleka kwenye mlima mrefu, na kusema, “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, nisujudie na kuniabudu, nitakupa falme hizi zote. Zote ni zangu, ninafanya nazo lolote nitakalo, nitakupa wewe, ikiwa tu utaniabudu.”

¹²² Yesu, akijua ya kwamba angezirithi katika ule Utawala wa Miaka Elfu, Yeye alisema, “Rudi nyuma Yangu, Shetani, kwa maana imeandikwa, ‘Utamsujudu Bwana Mungu wako, umwabudu Yeye peke yake.’” Ndipo Shetani akarudi nyuma Yake.

¹²³ Kuna methali ya kale ambayo ni zaidi ya methali, “Haidhuru ni vipi, ni nani aliyetangulia, inakubidi kutii kanuni za mchezo, la sivyo hutashinda kamwe.” Kama mkimbiaji anakimbia kwenye uwanja wa mbio, na mmoja achukue njia ya mkato, na kukatia uwanjani, na kumshinda huyo mwingine hapo kwa nusu saa, bado ataondolewa mwishoni mwa hayo mashindano. Hana budi kufuata kanuni za mchezo, la sivyo anaondolewa.

¹²⁴ Na hivyo ndivyo inavyotubidi kufanya, mbio za maisha tunazokimbia sasa, hazina budi kucheza kulingana na masharti ya Mungu, la sivyo tutapoteza tutakapofika kule. Kama sisi ni Rais, kama sisi ni Gavana, ama mhudumu, ama ni nani, sisi ni wa kanisa gani, ama ni wa dhehebu gani, kanuni za mchezo hazina budi kufuatwa, hatuna budi kuuendesha kwa haki, lazima tuucheze kwa kanuni; hatuna budi kuhubiri Neno, hatuna budi kufanya hivyo kwa hiari.

¹²⁵ Paulo alisema katika, ninaamini katika Waebrania mlango wa 12, “Kwa kuwa tumezungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ituzingayo kwa upesi, ili tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele zetu.” Paulo alikuwa akinena juu ya Olimpiki, na kadhalika, iliyokuwa katika Uyunani na Rumi, na kadhalika, alijua ya kwamba ilikubidi kucheza mchezo huo kwa haki, kwa kuwa kama hukufanya hivyo, ungeondolewa.

¹²⁶ Na usiku wa leo, kama Wakristo waliozaliwa mara ya pili, kama waaminio hapa kwenye wakati wa mwisho, inatubidi kucheza mchezo kulingana na kanuni. Hatuna budi kupiga mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele zetu, tukimtazamia Mwenye kuanzisha na Mwenye kutimiza, Yesu Kristo.

¹²⁷ Mara baada ya hayo, ama, kabla ya hapo, kabla ya hapo, alitoa ile sura kuu ya 11 ya Waebrania, ambayo inawaorodhesha wale mashujaa wa imani, “Kwa imani Musa; kwa imani Ibrahimu; kwa imani Henoko; kwa imani Nuhu,” mashujaa wote wakuu wa imani. Kisha kusema, “Kwa kuwa tumezungukwa na

wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi,” kutokuamini, “ituzingayo kwa upesi.”

¹²⁸ Sisi hapa usiku wa leo, moja kwa moja katika vivuli vya Kuja kwa Mwana wa Mungu, na hata hivyo, tunaona kanisa katika hali ya upungufu wa damu, tunapaswa kuwa mashujaa wakuu, wenye nguvu, hodari wa imani, ambao wangelitikisa taifa. Mungu na atupe sisi, laiti tungaliipokea! Ili kwamba mambo hayo juu yetu yanayotuzuia kukimbia, hebu na tuweke kando hiyo mizigo yote midogo sasa, kwa sababu tunamtazamia Mwenye kuanzisha na Mwenye kutimiza imani yetu, Yesu Kristo, Yeye aliyefanyika mtu duniani, akakaa kwetu, na akafanyika dhambi, ili kwamba kwa njia ya haki Yake tupate kusamehewa dhambi zetu.

¹²⁹ Alifanyika sisi, wenye dhambi, tupate kuwa haki Yake. Kwa maneno mengine, namna hii: Yeye alifanyika mimi, ili nipate kufanyika Yeye. Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, nilikuwa mwenye dhambi, alipachukua mahali pangu, akawa mwenye dhambi ili nipate kuwa Mwana wa Mungu. Na tunapoonam jambo hilo, linapaswa kuvutia usikivu wa kila mwanamume na mwanamke kuweka kando kila mazungumzo madogo ya shaka. Loo, ninapenda hilo! “Weka kando kila mzigo, na maskini kutokuamini ambako hutuzinga kwa upesi.”

Kitu fulani kidogo kikitokea, nasi tunasema, “Vema, sijawahi kusikia hilo hapo kabla.”

Lichunguze katika Maandiko, kama ni Biblia, dumu nalo.

¹³⁰ Ninyi watu hapa mnajulikana kwa matofaa yenu, matofaa makubwa matamu yanayokuzwa bondeni hapa, na matunda mengine. Unapouweka huo mti mdogo nje, si mkubwa kuliko *hivyo*, chipukizi dogo tu, kila tofaa litakalopata kuwa kwenye mti huo liko ndani yake papo hapo. Bila shaka, ndivyo, kama sivyo, yanatoka wapi? Yako ndani ya huo mti.

¹³¹ Nawe unaupanda huo mti ardhini, unaumwagilia maji, unautia maji, mti huo mdogo unafanya nini? Unakua, na mbona, jinsi unavyokua, unakunywa, na kuvuta kutoka ardhini, maji. Unavuta zaidi ya kipimo chake, zaidi ya kutosha kuuja, unavuta kiasi fulani mpaka unasukuma nje viungo, matawi, matofaa, kisha unashuka na kujificha wakati wa baridi kali, kuzuia utomvu usiuawe kwenye mti. Ni *Akili* gani inayoungiza ardhini, ukauficha kupitia majira ya baridi kali?

¹³² Hebu weka maji kwenye kikombe cha bati na uyaweke kwenye ua, uone kama yatashuka majira ya baridi kali yajapo. Bila shaka, hayatashuka, *Akili* fulani huushusha chini. *Akili* ile ile inayoyatelemba maji mle ndani, ni Roho yule yule wa Mungu aliyetuleta pamoja kwa ajili ya mkutano huu, Roho yule yule anayetuleta pamoja hapa chini ya ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, kupata wema Wake na rehema kwa ajili ya saa zilizo mbele yetu. Loo, Yeye ni halisi, Mungu ni halisi.

¹³³ Sasa, tunaona ya kwamba katika mti huu mdogo, unasukuma nje, unapokua unasukuma nje. Basi unapozaliwa katika Ufalme wa Mungu, mtoto mchanga tu katika Kristo, kila kitu unachohitaji katika safari ya maisha haya kiko ndani yako unapompokea Roho Mtakatifu. Loo, basi linalokupasa kufanya ni kunywa, na kunywa, na kuendelea kunywa. Usisimame tu unapojiunga na kanisa na kubatizwa, endelea tu kunywa mpaka uwe na imani kwa ajili ya *hili*, na imani kwa ajili ya *lile*, na imani kwa ajili ya *hili*, na kusukuma nje, mpaka madhihirisho yote ya Roho Mtakatifu yanaishi ndani ya Kanisa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] "...na Mpaji thawabu wale wamtafutao kwa bidii."

¹³⁴ Sasa, tunapandwaje? Tumepandwa katika Kristo Yesu. Sasa, ninaamini, haya ndiyo makadirio yangu kumhusu Yeye: Yeye ndiye Chemchemi ya Uzima isiyoisha, hata huwezi kuumaliza wema Wake. Baadhi ya watu wanafikiri, "Loo, ninachukia kumwita Mungu sana." Hivyo ndivyo anavyokutaka ufanye.

¹³⁵ "Hamna, kwa sababu hamwombi; hamwombi, kwa sababu hamwamini. Ombeni kwa wingi, furaha yenu iwe timilifu." Hivyo ndivyo Mungu anavyotaka, kuomba mambo makubwa. Ninaomba kwa ajili ya mamia ya watu katika mkutano huu. Ninaomba ya kwamba kila mgonjwa, anayeingilia mlango huo atatoka hapa akiwa mzima. Ninaliamini. Ninaamini ya kwamba baada ya sisi kwenda, ya kwamba haitakuwa tu ni kukusanyika kwingine, bali itakuwa ni uamsho katika Yakima hapa. Shetani ameniweka nje yake muda mrefu vya kutosha, nami ninaamini saa imewadia kwa ajili ya uamsho halisi, unaonea sana katika kila kanisa na kote nchini.

¹³⁶ Nilitoka alasiri ya leo, nikaenda mahali mbalimbali nikiwatembelea watu, nimevaa maskini kofia ya majani makavu, imeinamishwa juu ya uso wangu, na kadhalika, mimi, kuona tu mtazamo wa watu, mna watu wazuri hapa, mna kitu cha kufanyia kazi. Hiyo ni kweli. Sasa, tunachopaswa kufanya ni kuanza kazi. Tuko hapa usiku wa leo kumchagua Bwana wetu Yesu kama Mfalme wetu moyoni mwetu, Gavana wetu, Mpaji wetu wa imani, Mungu wetu, Mponya wetu, Mwokozi wetu. Kumchagua Yeye moyoni mwetu, na kutoka hapa nje sasa, na kulipeleka kwenye uchaguzi huu mkuu unaokuja kwenye Hukumu, wakati atakapovikwa taji Mfalme wa mfalme, na Bwana wa bwana.

¹³⁷ Sasa, tunaishi katika siku ya kutisha sana, lakini yote unayohitaji tayari umepewa unapoamini. Watu wengi sana, siku hizi, ninaona, wanapojiunga na kanisa, na hapa, hasa sana Marekani, wanakuwa tu wazururaji, wao tu ni, "Vema, Mungu asifiwe, nilikutana na Ndugu Branham, nami ni—nikaokoka, na nikaandika jina langu kwenye kitabu, na hayo—hayo ndiyo yote niliyofanya."

¹³⁸ Kuelea tu, hatutaki kufanya hivyo. Kamwe hukuokoka kusudi tu uwe mfuasi wa kanisa, uliokolewa upate kufanya kazi. Hatuliviki jeshi nguo ili tu kukaa pembeni na kubembana na wasichana, huku wamevaa sare nzuri, tunalifundisha jeshi letu kupigana vita. Wala hatuko mandarini, tuko kwenye uwanja wa vita, tuko hapa nje tukimkabili adui wa Bwana wetu Yesu, na adui wa nafsi zetu. “Na tuamke na tufanye tukijiepusha na ugomvi wowote.”

¹³⁹ Ninaipenda hiyo *Zaburi ya Maisha*, “Msiwe kama ng’ombe bubu, wanaosukumwa,” inawabidi kusukumiwa kwenye boma dogo mahali fulani, upande *huu*, na kushuka *huku*. Hebu tuwe shujaa!

Maisha ya watu mashuhuri yote
yanatukumbusha

Tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
Tunapotengana, tunaacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu;

Kumbukumbu, ambazo labda mwingine,
Huku akisafiri kwenye bahari kuu ya maisha,
Kwa ndugu mnyonge aliyeharibikiwa na meli,
Katika kuziona nyayo zetu, atajipa moyo tena.

Hebu tufanye jambo fulani, sisi ni nyaraka zilizoandikwa.

¹⁴⁰ Sasa, hapa siku moja, miaka michache iliyopita, mke wangu, nilikuwa kwenye chumba cha kusomea, akaja mlangoni, naye akasema, “Billy, kuna—kuna ombaomba mlangoni, anataka chakula.”

Nikasema, “Mlishe, mpe kitu. Yeye ni mwanadamu, sijali kile alichu, mlishe. Mgawie tulicho nacho, huyo mtu ana njaa.”

Akasema, “Ninamwogopa.”

Nikasema, “Loo, jamani! Fungua mlango na umwambie achukue chakula. Mpikie kitu, mpe.”

¹⁴¹ Kwa hiyo, akakiweka mezani, kisha akamwalika ndani, ndipo akaja chumbani. Kwa hiyo mimi, kidogo alimwogopa, kwa sababu kwa namna fulani alionekana mchafu, basi nikatoka, nikasema, “U hali gani, mtu wangu mwema?”

Akasema, “U hali gani?” Naye alikuwa akila chakula chake cha kutwa.

Na kwa hiyo, nikasema, “Unatoka wapi?”

Akasema, “Loo, hapa na pale tu.”

Nikasema, “Unaenda wapi?”

Akasema, “Loo, jambo lile lile, hapa na pale tu.”

Nikasema, “Una kusudi gani maishani?”

Akasema, “Hamna.”

¹⁴² Vema, hivyo ni karibu tu jinsi ambavyo—ambavyo watu huingia. Hatuna budi kuwa na kitu ambacho tunakusudia, hatuna budi kukusudia moyoni mwetu, hatuna budi kufanya jambo fulani.

¹⁴³ Sasa, kama ukisema, “Loo, tuna uamsho. Naam, tuko kwenye Ukumbi wa Shule ya Eisenhower,” usiache huyo awe ni wewe, mtu anayeelea tu na kuchukuliwa na mkondo, kamwe huwezi kuwa chochote kwa njia hiyo. Hebu tuamke na kufanya jambo fulani kulihusu, hebu tufanye jambo. Hebu tuone ya kwamba kanisa letu linafanikiwa, hebu na tuufanye Ufalme kufanikiwa, hebu tuone kwamba wagonjwa wanaingia humu ndani, hebu tuone ya kwamba Mungu anaabudiwa miongoni mwa watu, na ishara kuu na maajabu yakitukia ambayo yataenea nchini. Nimeridhika kwamba kutakuwa na mambo yatakayotukia hapa ambayo yataifurahisha nchi hii, ambayo yataitikisa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, kama kila mmoja wetu atakuwa nyuma yake.

¹⁴⁴ Tunafanya nini? Kumjengea jukwaa Bwana wetu. Tunataka kumleta Yakima, tunataka kumleta katika uamsho mkuu. Nasi hatuna budi kumchagua moyoni mwetu wenyewe, hatuna budi kukusudia kitu fulani, kupata kitu cha kufanya nacho, kitu cha kufanya, kusudi fulani. Huninii tu, loo, kujiunga na kanisa na kuelea, hufanyi hivyo, daima, huna budi kuwa na kusudi katika yale unayofanya.

Mke anasema, “Vema, mimi ni mke tu.”

Nenda kwenye simu, fanya jambo fulani. Fanya kitu cha kumsaidia Bwana Yesu, sasa.

¹⁴⁵ Sasa, kuna wakati ambapo mtu anaweza kufikia mahali ambapo anaweza kuwa na kusudi, ni kitu kitakachombadilisha, na hapo ni, wakati mtu anapokutana na Mungu. Mtu hawezi kuwa vivyo hivyo akiisha kukutana na Mungu uso kwa uso. Itambadilisha licha ya chochote unachoweza kufanya juu yake; mtu kamwe hawezi kuwa vivyo hivyo baada ya kukutana na Mungu. Sasa, hiyo ni kweli.

¹⁴⁶ Hebu na tumchukue mtu fulani, kulikuwako na Nuhu, Nuhu hakuwa na kusudi halisi maishani, alikuwa mkulima wa kawaida, huko nje kondeni, ndipo siku moja Mungu akakutana naye, na akasema naye, na kumwambia jambo fulani lisiloweza kutukia kamwe, lingetukia, basi tangu saa hiyo na kuendelea, mbona, Nuhu akakusudia moyoni mwake ya kwamba angeijenga safina hiyo, haidhuru washupavu wote wa dini walisema nini.

¹⁴⁷ Mbona, mvua haikunyesha kamwe kutoka mbinguni, kamwe hawakuwa na unyevu wowote juu ya nchi, ilimwagiliwa maji kutoka kwenye chemchemi, hakukuwahi kuwa na wingu angani. Alikuwa atafanyaje jambo hilo? Vema, Mungu alisema litatukia, naye Nuhu akakusudia moyoni mwake kufanikisha jambo hili

kwa ajili ya Mungu, naye akalifanikisha, haidhuru walimcheka kiasi gani, ama ni kiasi gani walisema *hivi, vile*, ama *vinginevyo*.

“Itanyeshaje? Mvua iko wapi, Nuhu?”

“Sijui.”

“Nionyeshe mahali mvua ilipo.”

“Siwezi kukuonyesha, lakini wakati utakapowadia, mvua itakuwepo.” Sawa. Alikutana na Mungu.

¹⁴⁸ Basi wakati daktari wako alipokukataa, na kusema, “Kansa itakuua.” Utaishije kamwe?

“Siwezi kuwaambia jinsi itakavyokuwa, lakini Mungu alisema, ‘Kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule,’ na itakuwa hivyo.” Sawa.

¹⁴⁹ Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikihubiri juu ya Eliya na wale kunguru wakimlisha, nikatoa tamshi dogo, fidhuli, watu weusi mniwie radhi kwa hili, lakini nilisema, “Alikuwa afadhali kabisa, walisema alikuwa mwendawazimu kule chini ya mti ule, alikuwa na watumishi weusi kumtumikia kila siku. Alipotaka maji, angenyosha mkono anywe; ilipofika wakati wa chakula, mtumishi mweusi, kunguru, akaja akamletea sambusa.”

Ndipo mhudumu wa kanisa fulani akaniambia, “Kwa kweli huamini kwamba hizo zilikuwa sandwichi?”

Nikasema, “Hakika ninaamini. Biblia ilisema ilikuwa ni nyama na mkate, nami ninaamini hivyo.”

Kasema, “Basi ninataka kukuuliza jambo fulani: Aliupata wapi? Hao kunguru waliupata wapi?”

¹⁵⁰ Nikasema, “Hilo halikuwa juu ya Eliya kuwazia hayo yote, alijua tu Mungu alimwambia angemlisha, kunguru wakauleta, akaula, na ameshiba kwake, na hilo tu ndilo muhimu.”

¹⁵¹ Hivyo ndivyo ilivyo kuhusu uponyaji wa Kiungu, ama nguvu za Mungu, haidhuru ni nani anayejaribu kuuelezea, na kuuonyesha, Mungu alisema itakuwa hivyo, na itakuwa. Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele; nguvu Zake ni zile zile. Yeye alisema, “Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya.”

“Utafanyaje jambo *hili*?”

“Siwezi kuwaambia, lakini Mungu alisema lingetukia, nalo linatukia tu, hilo tu ndilo nijualo.”

¹⁵² Siwezi kueleza jinsi ng’ombe mweusi anavyoweza kula majani ya kijani kibichi, na kutoa maziwa meupe, bali ninayanywa wakati wote, vivyo hivyo tu. Sijui mitambo yake, lakini kitu pekee nijuacho ni maziwa, nami ninayanywa. Hiyo ndiyo njia . . .

153 Mtu fulani alisema, “Loo, unawachochea hao watu sana, wote wamesisimkwa. Hiyo...”

Sijui kuhusu hilo, siwezi kusema ni msisimko wa aina gani, ninajua ya kwamba kitu fulani kilibadilisha maisha yangu, wakati msisimko huo uliponijia.

Mtu fulani alisema, “Utaingia kichaa.”

154 Nikasema, “Niche basi, nina furaha zaidi namna hii, kuliko nilivyokuwa vinginevyo.” Kwa hiyo, nilipata wokovu namna hii. Natumaini nitakaa na msisimko mpaka nife, kwa sababu nina wakati mzuri sana nikiliamini Neno la Mungu, na kumwona Yeye akilithibitisha kwa kila kitu alichosema aliahidi kufanya. Huyu hapo Ndiye Bwana wetu, huyo ndiye Yule mkuu, hakika, tunaamini.

155 Loo, Mungu anapokutana na mwanadamu, anabadilika. Nuhu alipokutana na Mungu, mafanikio yake yote yalikuwa ni kuijenga hiyo safina.

Watu wakatoka, “Unafanya nini, Nuhu?”

“Najenga safina.”

“Safina ni nini?”

“Ni mtumbwi.”

“Mtumbwi ni nini?”

156 “Ni kitu fulani, maji yanakuja, yatatiririka kutoka mbinguni, naye Mungu atauangamiza maskini ulimwengu huu mwovu, na wote wasioingia katika safina hii wata—wataangamia.”

“Aa! Aisee, nyote mnapaswa kumpeleka kwa mtaalamu wa magonjwa ya akili, kuna kasoro kichwani mwa mzee huyo.”

157 Vema, ilikuwa ni nini? Alimwamini Mungu. Na mtu anayemwamini Mungu, anatenda kipumbavu kwa ulimwengu, kwa sababu ilimpendeza Mungu kwa upumbavu wa kuhubiri... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... tai. Amina.

158 “Wote wanaoishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu watateswa. Heri ninyi, watu watakapowashutumu na kuwafanya mzaha wa kila namna, na kuwaita majina ya kila namna, kwa ajili Yangu.” Mnaona? “Furahini na kushangilia sana, maana waliwatesa manabii waliowatangulia.” Daima imekuwa hivyo. Unapopata roho ya taifa hapa juu yako, unakuwa Mmarekani. Hiyo ndiyo roho nzuri ya kitaifa ya kuwa nayo, lakini wakati mwingine kutokana na jinsi mambo yanavyoendelea sasa, inazidi kuwa mbaya sana.

159 Nilikuwa huko Sant’Angelo, hivi majuzi tu huko Rumi, na ubao mkubwa kabla hujaingia Sant’Angelo ulisema, “Kwa wanawake wa Marekani: Tafadhali vaeni nguo kuwaheshimu wafu, kabla hamjaingia humu.”

¹⁶⁰ Unafikiri hiyo ni mbaya sana, kiongozi mkuu wa taifa fulani, baada ya sisi kumaliza, alisema, “Je, nyote mna wanawake wazuri nchini mwenu?”

Nikasema, “Maelfu yao.”

“Vema, kwa nini mnaimba hizo nyimbo zote chafu juu yao? Kila wimbo unaokuja hapa, kitu fulani kichafu kuhusu wanawake.”

¹⁶¹ Nikasema, “Huo ni upande huo mwingine tu, hujui upande wake mzuri. Unasoma ule ukurasa mtupu.” Lakini nikasema, “Sisi, hakika, tuna wanawake Wakristo waliozaliwa mara ya pili, ambao ni wanawake waaminifu na halisi, vijana kwa wazee, halisi, wao ni watu wa Ufalme.” Kwa kweli, nilisema, “Kwa hiyo nilienda nchini mwenu kukwaambia habari zao.” Sawa. Mnaona? Unapopata roho!

¹⁶² Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa ninaenda dukani, mimi na mke wangu, na kulikuwa na hawa akina mama wakitembea na maskini nguo hizo za kizinifu, wa—wala hatukuona ila yapata mwanamke mmoja kati ya yapata elfu kadhaa aliyekuwa amevaa nguo za aina nyingine yoyote. Ndipo—ndipo mke wangu akaniambia, kasema—kasema, “Billy, ni—ni kitu gani kinachowafanya wanawake wote wavalie namna hiyo.”

Nami nikasema, “Loo hiyo ni roho tu ya Kimarekani, hivyo tu.”

“Vema,” kasema, “kwani sisi si Wamarekani?”

Nikasema, “Naam, sisi ni Wamarekani. Hiyo ni kweli. Taifa kuu kuliko yote ulimwenguni, tunalipenda, lakini hata hivyo, sisi si Wamarekani hasa.”

Kasema, “Sisi ni nani?”

¹⁶³ Nikasema, “Tumezaliwa Mbinguni.” Nikasema, “Tulipopanda Kule juu... Sasa, kama wewe ni—ni Mmarekani tu, ungeweza kuvaa kama hao wengine wafanyavyo, na ufuata mkondo ule ule, uchukuliwe, uelee moja kwa moja pamoja nao. Lakini wakati Roho yako inatoka Huko juu, ni takatifu. Haleluya! Ni tofauti. Inakufanya utende kama wafanyavyo Huko juu.” Hiyo ni kweli. Kwa hiyo unapompokea Roho huyo, unakuwa wa kipekee kwa watu hawa hapa, unaona, unaonekana tofauti, unatenda tofauti.

¹⁶⁴ Na hivyo ndivyo Nuhu alivyofanya. Alikuwa amenena na Mungu, naye alikuwa amebadilishwa kutoka mzururaji tu katika ule ulimwengu uliotangulia ile gharika, akawa kiumbe cha Mungu kilichokuwa kimezaliwa katika Ufalme kipate kuleta Ujumbe.

¹⁶⁵ Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Dini kama ya kilokole, watu wanaishi kitakatifu, wakidai kuna *kitu fulani* kinachotoka Juu, nasi tunaamini si maji, bali

Maji ya Uzima yanaanguka kila usiku kutoka Juu, kutoka kwenye Chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya ile Gharika, wanapoteza mawaa yao yote ya hatia. Nguvu na utukufu hutiririka kutoka kwenye Chemchemi hiyo huko juu hadi kwenye Kanisa Lake. Alipokufa, na kufufuka kwenye asubuhi ya Pasaka, alikuwa ametoboa shimo kote kwenye pande za Utukufu kuacha utukufu ulishukie Kanisa Lake lililokuja kwenye Siku ya Pentekoste, umekuwa ukianguka tangu wakati huo. Tunaamini hilo kwa mioyo yetu yote.

¹⁶⁶ Sasa angalieni, tunapoweka jukwaa Lake, hebu tumchukue mtu mwingine kwanza. Kulikuwako na Ibrahimu, alikuwa tu ni mtu wa kawaida, alishuka pamoja na baba yake kutoka huko Babeli, na Shinari, huko chini bondeni, na kuishi huko katika mji wa Uru, katika nchi ya Ukaldayo. Na muda si muda mwajua, labda alikuwa ni, loo, mtu wa kondeni, ama mchungu kondoo, ama kitu fulani, basi siku moja alikuwa huko nje kondeni alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, mke wake, Sara alikuwa na sitini na mitano, ndipo Mungu akakutana na Ibrahimu na kumwambia juu ya Nchi nyingine iliyokuwa mbali sana na hiyo.

¹⁶⁷ Naye akamwambia atapata mtoto kwa Sara, naye alikuwa amepita umri wa kuzaa, na alikuwa tasa maishani mwake mwote, na, loo, mume alikuwa, pia, lakini ni nini kilichokuwa kinaenda kutukia? Mungu alikuwa anaenda kutekeleza jambo fulani. Na mtu huyo mwaka baada ya mwaka, maadamu aliishi, alikiri kwamba alikuwa msafiri na mgeni, akiutafuta Mji ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu. Amina. Inambadilisha mtu anapomsikia Mungu akisema naye.

¹⁶⁸ Loo, sikiliza juma hili, isikilize Sauti ya Mungu ikisema nawe, itakubadilisha, itakuondolea shaka lote moyoni mwako, tukijua ya kwamba Yesu wetu ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tunapomwona akiya mikutanoni, akianza kufanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani, ndipo unataka kuisikiliza kwa makini ile Sauti ndogo, Kitu fulani kile kitakachokubadilisha, na kusema, "Naam, Mungu, hivyo ndivyo hasa Maandiko yasemavyo, hilo ni Neno kwa Neno yale Maandiko yasemayo."

¹⁶⁹ Uende nyumbani, uchukue Biblia yako, utoe hoja, uone kama ni kweli, uyachunguze Maandiko, halina budi kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, likiambatana na Biblia. Hiyo ndiyo ahadi yako hasa, basi msikie Mungu, itakubadilisha, itakupa imani ya kuamini. Hiyo mikono iliyolemaa itanyoka, miguu hiyo itanyoshwa, hiyo kansa itatoweka, hayo macho mapofu yatafunguka, na mambo ambayo Mungu aliahidi yatadhihirishwa.

¹⁷⁰ Tuko katika ulimwengu ambao umeachishwa mambo hayo,

bali tunajenga jukwaa usiku wa leo kwa ajili ya Mtu. Amina. Mtu! Kama yule mwanamke alivyosema, kisimani, “Njoni, mwone Mtu, aliye niambia mambo niliyotenda. Je, haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?”

¹⁷¹ Njoni, mwone Mtu, Mtu tunajenga juu yake usiku wa leo, Bwana Yesu, juu Yake, kwa maana juu ya misingi mingine yote ni mchanga unaodidimia. Misingi mingine yote itaangamia, bali Mwamba huo, Kristo Yesu, utasimama milele. Mnaamini hilo?

¹⁷² Naam. Ibrahimu alikiri ya kwamba alikuwa msafiri na mgeni. Siku zote za maisha yake aliutazamia Mji huo, ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni alikuwa ni Mungu; daima hivyo.

¹⁷³ Musa alikuwa ameondoka Misri, na alikuwa amefika nyikani, alikuwa akiishi vizuri, alikuwa akiishi nyuma ya mlima, mke mzuri, mvulana mdogo, Gershomu, kuwa mrithi wa kondoo wote wa Yethro, naam, mbona, alikuwa sawa, alikuwa akienda, akipeperushwa tu na urahisi wa mawimbi. Israeli huko chini katika matatizo, wakilia, huku Mungu alikuwa amemchagua kuwakomboa watu, bali alikuwa amejiondoa kwa hilo.

¹⁷⁴ Sasa, hiyo ndiyo shida ya mengi ya makanisa yetu siku hizi. Mungu alituita kwenye huduma, Mungu alituita kuwa watu Wake, Mungu alituita kuamini ishara na maajabu, Mungu alituita kufanya ishara na maajabu, Yeye alituita kufanya hivyo, nasi tunaenea mbali sana na jambo hilo. Tunachohitaji ni kutembelewa tena na Mungu. Ee Mungu utume hapa kwenye Ukumbi huu wa Eisenhower! Tuma kuzuriwa na Roho wa Mungu!

¹⁷⁵ Tunaenea mbali sana kama Musa alivyofanya. Musa alikuwa sawa huko nyuma, alikuwa na maisha mazuri. Kanisa siku hizi lina majengo makubwa kuliko liliyowahi kuwa nayo, makanisa bora, watu waliovalia vizuri zaidi, watu walio na maisha bora kuliko liliyowahi kuwa nao, lakini, loo, ndugu, jambo si hilo, mambo hayo huangamia. Hatuna budi kupata *ushindi*, hatuna budi kupigana, hatuna budi kufanya jambo fulani kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

¹⁷⁶ Huyu huko nyuma Musa akiishi kwa anasa, akishuka kwenda asubuhi moja, ndipo Mungu akanena naye kutoka kwenye kile kichaka kilichowaka moto, mtu huyo alibadilishwa tangu wakati huo na kuendelea. Ni jambo la kimapinduzi jinsi gani linalokufanya ufanye wakati wowote unapomwona Mungu! Mwangelie Musa, kakimbia, akamwua Mmisri mmoja, kisha akatoroka akaenda jangwani, naye huyu hapa kesho yake asubuhi, baada ya kukutana na Mungu katika kichaka hiki kilichowaka moto, alikuwa na mke wake ameketi kwa kutagaa juu ya nyumbu pamoja na yule mtoto Gershomu kwenye nyonga yake namna *hiyo*, masharubu yakining'inia chini *hivi*, ameshika fimbo mkononi mwake, akienda kule, akiyumbayumba tu,

akipaza sauti tu na kumsifu Mungu, akimwongoza maskini nyumbu huyu aliyembeba mke wake.

“Unaenda wapi, Musa?”

“Nashuka kwenda Misri kuiteka.” Uvamizi wa mtu mmoja, bali aliiteka. Aliiteka kwa sababu Mungu alisema hivyo, naye alikuwa na imani.

¹⁷⁷ Mungu anapozungumza na mtu, yeye ana imani, na ana shauku, na ana kusudi. Mungu anapozungumza na mtu, inampa kusudi; Mungu anapozungumza na mtu, inampa shauku; Mungu anapozungumza na mtu, inampa imani ya kulifanya, kutimiza, ama kufanikisha kilicho kusudi lake maishani, yale Mungu amemwitia kufanya.

¹⁷⁸ Ametuita tupate kuwa Kanisa la Mungu, amina, hebu—hebu tulifanye tu kusudi letu maishani kuona kwamba sisi ni Kanisa la Mungu. Hebu na tuwe na shauku, sio kukaa huku ati kwa sababu akina Jones wanataka, ama ninii—ama ninii...?... taka. Tunajali nini kuhusu...?...wasipofanya hivyo, hebu na tulifanye, kwa vyovyote vile. Kama taifa lote linataka kuzama, hilo ni juu yao, katika Yakima tunamtetea Mungu, tunamtaka Mungu, tunataka kufanikisha, tunataka kuwa na imani, tunataka kuwa na lengo.

¹⁷⁹ Hebu tumwamini Bwana Yesu Kristo, kwa kuwa Yeye alisema, “Mambo yote yanawezekana kwao waaminio. Amin, nawaambia,” si *kama Mimi*, bali, “*kama wewe* ukiuambia mlima huu, ng’oka, wala usiwe na shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba hayo uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote. Unaamini hilo?

¹⁸⁰ Alikuwa na shauku, kamwe hakuwa vile vile baada ya hapo. Alikuwa na shauku, alikuwa na jambo la kufanyia kazi, naye alikuwa na imani ya kuifanya. Siku zote za maisha yake alimtumikia Mungu kuwakomboa watu hao. Hakujali maadamu alikuwa anaendelea vizuri, alijali nini kuhusu hao watu waliokuwa wamelala pale chini wakiteseka. Ndipo Mungu akasema, “Nimesikia kilio cha watu Wangu, nami ninakumbuka ahadi Yangu pamoja nao, pamoja na Ibrahimu.”

¹⁸¹ Na leo hii, wakati kanisa linaugua, maradhi yanalundikana, na watu kwa sababu ya—ya kiburi cha kiakili, na kadhalika, wanaachana na uponyaji wa Kiungu, wanaachana na Roho Mtakatifu, Mungu angali anasikia kilio cha watu Wake, mtu fulani hana budi kwenda.

¹⁸² Yakima, hebu na tuinuke na kuangaza katika Jina la Bwana Yesu. Kama wewe ni mgonjwa, sema, “Mimi ni mgonjwa mwilini.”

¹⁸³ Mungu amenena, Mungu alisema hivyo, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, katika Jina Langu wataweka

mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Mungu amenena. Una shauku?

“Vema, daktari alisema nitakufa.”

¹⁸⁴ Hivyo ndivyo vizuri zaidi daktari ajuavyo, amesoma, kila utafiti wa tiba unaonyesha ya kwamba amefanya yote awezayo kukufanyia, kwa hiyo kulingana na sayansi ya tiba utakufa, lakini, “Kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa huyo.” Ipandishe shauku yako, uwe na kusudi kwamba utaponywa kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kisha uje na imani ya kwamba “Nitaupokea,” nawe utaupata. Naam, bwana.

Unasema, “Ndugu Branham, siwezi kulielewa.”

¹⁸⁵ Vema sasa, ninapoenda—ninapoenda ng’ambo, nami ninapanda hapa juu, hii hapa meli kubwa imeketi hapo, chombo anga kikubwa, kuzunguka mara saba, ni—nimeruka kote kwa kitu hiki, sipandi juu na kusema, “Aisee, Rubani, kabla sijaingia kwenye meli hii, hebu niambie ni darubini ngapi, kila moja ya hiyo mihimili inazo, nielezee kimitambo jinsi ndege hii yote itakavyofanya kazi. Katika wakati wa dhoruba, itafanya nini? Una nguvu kiasi gani? Unaweza kupanda juu kiasi gani? Mbinu zote.” Mimi siulizi mambo hayo yote. Ninajua hiyo meli ilivuka na mtu mwingine, na kama hiyo meli ilivuka na mtu mwingine, itavuka na mimi. Kwa hiyo ninaipanda tu, na kujipatia kiti, na kuketi chini, ni juu ya rubani kuhakikisha kwamba ninafika kule.

¹⁸⁶ Hivyo ndivyo ilivyo kwa uponyaji wa Kiungu, sijui mbinu zake zote, siwezi kuwaambia mbinu zake, hakuna mtu mwingine anayeweza. Jinsi Mtu anavyoweza kufia huko na kuchapwa mgongoni Mwake, kama Yeye ni Mungu sana hata akawaponya wagonjwa, kwa sababu anaamini hilo, siwezi kueleza hilo, sijui mbinu zake, ninashika tu ahadi na kuikubali, na kusema, “Bwana, ni kweli.” Hilo latosha. Mnaamini hilo, sivyo, ndugu? Hakika. Likubali tu kwa msingi kwamba Mungu alisema hivyo; huyo ndiye Mtu tunayemjengea jukwaa.

¹⁸⁷ Tamshi sasa kabla ya kufunga, huenda nikasema hivi: Vipi kuhusu wakati unapojisalimisha kwa daktari? Daktari anapokuja, naye anasema ana dawa kwa ajili yako, nawe unachukua hiyo dawa, unasema, “Sasa, Daktari, keti hapa chini, na, uniambie vyote vilivyo kwenye kidonge hiki. Mimi—mimi. . . Mbinu zake ni zipi? Uchambuzi wote wa kidonge hiki ni nini? Umenichanganyishia fomula ya dawa gani hapa? Ulipataje sumu hii kali? Walifanyaje. . . ? Hiyo ilifanywaje? Ilitokana na nini? Ni nani aliyeivumbua? Na gliserini hii ilitoka wapi? Navyo hivi, vitu hivi vyote vinavyoingia kwenye fomula vilitoka wapi?”

¹⁸⁸ Yeye anaandika katika Kiyunani, labda hata yeye mwenyewe hajui, anaandika tu. Vema, hivyo ndivyo alivyoambiwa afanye. Lakini jambo pekee ufanyalo, unamtii daktari na kumeza hicho

kidonge, hivyo tu. Na kama unamwamini daktari wako, kuna uwezekano, itakusaidia.

¹⁸⁹ Hilo ni jambo lile lile kuhusu kunywa hiki *Kidonge-Injili*, siwezi kuwaambia yote kukihusu, bali ninajua kinafanya kazi; ninaona ukimeza vingine. Itakapofika wakati wa kufa, utahamishwaje, uende kwenye ulimwengu mwingine, na kuwa kiumbe kipya kule, na—na usizeeke, ugeuke uwe kijana tena? Utaendaje kule? Sijui. Ninajisalimisha tu kwa Rubani wangu kwenye siku ya kuondoka kwangu, Yeye atahakikisha ya kwamba ninafika kule vizuri, Yeye atayashughulikia hayo mengine.

¹⁹⁰ Mabega yangu yatanyoka tena, nami nitakuwa kijana mwanamume, na nitakuwa tofauti basi. Mnaona? Kwa sababu ishara zote za mauti zitaondolewa kwenye maskini mwili huu, nami nitafanywa, nitakuwa na mwili kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, kwa kuwa nitamwona jinsi alivyo.

¹⁹¹ Sisemi, “Bwana, niambie jinsi unavyofanya jambo hilo.” Sijali jinsi unavyofanya jambo hilo, maadamu ninalo, hilo ndilo jambo muhimu. Naye aliahidi jambo hilo, nami ninaliamini. Amina.

¹⁹² Alituahidia uamsho, aliahidi ya kwamba ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule; sijui mbinu zake, yote nijuayo, Yeye aliahidi hilo, na ni kweli. Nimewaona wengine wakilikanyaga na kuvuka, basi ninaweza kulikanyaga, pia, na kuvuka, nawe unaweza kulikanyaga na kuvuka.

¹⁹³ Vipi kama daktari akija, na kusema, “Una kidole tumbo ninachopaswa kutoa,” ama, “Sina budi kuondoa bo—bonge la damu ubongoni.”

“Vema, Daktari, niambie tu, ni mishipa mingapi? Inakubidi kukata nini? Unalikataje *hili*? Vipi...?”

¹⁹⁴ Hufanyi hivyo, unaninii tu, wewe ni mgonjwa na unataka kupona, kwa hiyo unajisalimisha tu kwa daktari, naye anaendelea na kufanya hiyo kazi, hakuna lingine. Hiyo ni, vivyo hivyo kuhusu Yesu Kristo.

¹⁹⁵ Loo, jamani! Natumaini, usiku wa leo, ya kwamba Yeye atafanya upasuaji mkubwa juu ya imani yetu sote. Hivi hamtumaini hivyo? Huondoa kidole tumbo kilichopasuka, vyote—vitu vingine vyote, maskini wala mizoga wanaotuzunguka, chaza, na kupitia masikitiko, na kadhalika, usiku wa leo. Acha tu Mungu aishughulikie imani yetu na kuondoa *yote*, aondoe kila kitu, na tunapouzindukia ukweli wa kujua ya kwamba Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, tutakuwa na imani kamilifu ya kufanya kazi katika juma hili lijalo.

¹⁹⁶ Mnaamini hilo, Kanisa la Mungu? Mnaamini ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Je, uko tayari kuukabidhi ugonjwa wako moja kwa moja mkononi Mwake? Utafanya hivyo? Utafanya yote uwezayo sasa, juu ya jukwaa hili la Mtu ninayejaribu kuzungumzia habari zake? Yeye ni Mwokozi wako, Yesu Kristo. Hivi utajikabidhi...? Je, u—utampigia kura, sasa hivi? Je, utamchagua Yeye, Mwokozi wako, Mponya wako, sasa hivi, moyoni mwako, na kusema, “Bwana Mungu, nitaamini kila Neno lake. Nitafanya kazi na yote yaliyo ndani yangu, na kila kitu kinaendelea, kama nikiona jambo fulani likiendelea mkutanoni juma hili, ambalo silielewi, nitaenda moja kwa moja nyumbani nione kama liko kwenye fomula, nitaenda moja kwa moja nyumbani, nione kama liko katika Biblia, nione kama Mungu aliliahidi?” Kama Yeye aliliahidi, ni—ni majaliwa yako kuliamini, ni kwa ajili yako, ni—ni fomula ambayo Mungu amekupa.

¹⁹⁷ Hivi majuzi usiku, nilikuwa nikihubiri juu ya somo la *Kwa nini?* Na, “Kwa nini? Kwa nini?” Nami nikawaambia Biblia ilikuwa na fomula, katika fomula hii mle ndani mlikuwamo na tiba ya dhambi na magonjwa. Je, ungetaka kuangalia katika wa Musa, mbona, alikuwa na... Mkoba wa Musa? Aliwahudumia Waisraeli milioni mbili, naye akawaweka mle kwa muda wa miaka arobaini, na walipotoka, hapakuwapo na mnyonge miongoni mwao.

¹⁹⁸ Kama kungekuwako na daktari hapa, hivi hungetaka kuona ni maelekezo gani ya dawa aliyokuwa nayo Musa? Ni watoto wangapi waliozaliwa kila usiku? Unaona? Musa alitoa maelekezo gani? Hakuwa na nyongeza ya damu, na kadhalika huko nje kwa ajili ya magonjwa haya mabaya, na—na inambidi kuzaa kwa kupasuliwa, na kadhalika. Fomula yake aliyokuwa nayo ni ipi? Mnataka kujua ni ipi? Imeandikwa papa hapa katika Mwanzo, ama Kutoka, hasa, imeandikwa hapa, “Mimi ni Bwana Mungu wako nikuponyaye magonjwa yako yote.” Hiyo ndiyo fomula aliyokuwa nayo.

¹⁹⁹ Huyu ndiye Mtu tunayetaka kumchagua katika huu, kwa ajili ya kampeni *yetu*. Wote wanaotaka kumchagua Yeye moyoni mwenu, ili kumpigia kura, awe Bwana wenu *aliyefufuka*, Mponya wenu *aliyefufuka*, Mungu wenu *aliyefufuka*, aliyewafia, na kufufuka tena siku ya tatu, na yu hai, hivi mtamchagua? Useme, “Bwana, ingia ndani ya jengo hili, kila usiku, ingia moyoni mwangu. Nipe imani na ujasiri, nipe shauku, nifanyie jambo fulani, ninataka kubarikiwa kwa nguvu Zako.” Inueni mikono yenu kama mtamchukua namna hiyo, msemi, kila mahali, popote mlipo. Bwana awabariki.

²⁰⁰ Sasa, kesho usiku, Bwana akipenda, watakuwa hapa kugawa kadi za maombi saa kumi na mbili u nusu. Na halafu tutaanza mstari wa maombi yapata saa mbili na nusu, yapata saa tatu

na nusu, nadhani, ama, saa tatu, na ifikapo saa tatu na nusu tutakuwa tumetoka.

²⁰¹ Sasa, nilifikiri usiku wa leo ningesema mambo haya, kujenga jukwaa dogo, kuwafanya mjue yale tunayoamini. Tunamwamini Yesu Kristo na kila ahadi aliyotoa; tunaamini ya kwamba Agano Jipya ni—ni mfano wa lile la Kale, kwamba linachukua tu kutoka kwa la Kale, lile la Kale lilikuwa kivuli cha Jipya, na mambo ambayo Mungu alifanya katika yote mawili, yapo hapa leo katika umbo la Roho Mtakatifu, Nguzo ile ile ya Moto, Mungu yeye yule, uponyaji ule ule, baraka zile zile, nguvu zile zile za kuokoa; kila kitu alichokuwa, ndicho alichio leo, na atakuwa milele. Nasi hatuamini ya kwamba mambo haya yako katika mwanadamu, tunaamini ya kwamba mwanadamu ana karama, bali Mungu tayari amenunua wokovu wetu, uponyaji wetu pale Kalvari.

²⁰² Nami nataka umchague Yeye moyoni mwako usiku wa leo useme, “Mungu, tuma nguvu Zako, tuma baraka Zako, nitaliamini na kulikubali kama mali yangu binafsi kutoka Kwako. Ni ahadi uliyonipa.” Bwana na awabariki.

²⁰³ Sasa, ninawatakeni mwekeane mikono sasa, kote jengoni, popote ulipo. Sasa, kama kuna mtu, hapa, ambaye ni mgonjwa na anayeteseka, Biblia imesema hivi: “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

Biblia kamwe haikusema, “Ishara hizi zitafuatana na Ndugu Branham, Ndugu Roberts, ama mchungaji wako, ama mchungaji wa mtu mwingine.”

“Ishara hizi zitafuatana na *hao*,” wingi.

Je, wewe ni mwaminio? Sema, “Amina.” Basi ishara hizo zitakufuata.

“Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

²⁰⁴ Unaamini hilo? Basi ninapowaombea ninyi nyote hapa, kila mmoja wenu, usijiombe mwenyewe sasa, mwombe mtu uliyemwekea mikono. Unaona? Sema, “Bwana, mpe mtu huyu niliyemwekea mkono wangu, wape haja ya moyo wao.” Sema hivyo. Sema, “Wape, kama ni wagonjwa, wape uponyaji.” Kama unamjua mtu huyo, sema, “Mponye mtu huyu.” Nazo nguvu za Mungu zitamponya kila mmoja wenu.

²⁰⁵ Na kesho usiku mtarudi hapa, mkisema, “Ndugu Branham, kabla jambo lolote halijatukia, kabla sijaona kazi yoyote kuu ya Roho Mtakatifu, tayari nimeshuhudia hilo maishani mwangu, kwamba Yeye aliniponya jana usiku, moja kwa moja tulipokuwa tukijaribu kumchagua Yeye nilimkubali moyoni mwangu, na jambo fulani likatukia. Nilininii tu—nilininii tu... Yeye alinifanyia upasuaji jana usiku, na mashaka yangu yote yamezikwa kwenye chemchemi, na sasa mimi ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu.”

²⁰⁶ Tunapoinamisha vichwa vyetu. Kukiwako na mwenye dhambi hapa, mkumbuke Muumba wako sasa, wakati unapoweza, kwa maana saa itakuja hivi karibuni ambapo hutaruhusiwa jambo hili. Mtu aliyerudi nyuma? Mrudie Mungu, usiku wa leo. Hivi hutafanya hivyo? Basi enda asubuhi na mapema kanisani, na useme, “Mchungaji, ninarudi sasa, nataka kuurudia ushirika wangu.”

²⁰⁷ Kama wewe ni mwenye dhambi, shuka uende kwenye kanisa ulilochagua, na useme, “Nibatize, Mchungaji. Ninataka kuwa mshirika wa kanisa. Ninataka kumtumikia Mungu.” Halafu kesho usiku nenda ukawachukue wenye dhambi wanne ama watano zaidi na kuwarudisha. Angalia uone kama Roho Mtakatifu haingii kwenye kusanyiko, amtoe Yesu Kristo kama tu alivyokuwa jana, leo, na hata milele.

²⁰⁸ Baba yetu wa Mbinguni, juu ya msingi wa Neno Lako, juu ya msingi wa Damu Yako iliyomwagika, juu ya mateso Yako makali pale Kalvari, ushindi Wako juu ya mauti, juu ya kuzimu, na kaburi, na juu ya Shetani, kazi zote za Shetani, kuanzia dhambi hadi ninii yake, sifa zake zote, kufikia magonjwa, na masikitiko, na fadhaa, na uchovu wote wa huzuni unaoambatana nao, mashaka yote na kadhalika, tulijenga jukwaa hapa, usiku wa leo, kwa ajili ya Mwanao mpendwa, Bwana Yesu.

²⁰⁹ Tunamchagua Yeye, Bwana, kwa ajili ya uamsho huu. Nasi tuna furaha, Bwana, hakuna mwingine tunayemtaka, hatutaki mtu yeyote ila Yesu, tunampenda, tunamwamini Yeye kwa moyo wetu wote. Tumemchagua Yeye kama Mwokozi wetu, hakuna mwokozi mwingine. Hakuna kanisa, hakuna kanuni ya imani, hakuna dhehebu, hakuna mchungaji, hakuna papa, hakuna kasisi, hakuna rabi, hakuna chochote kinachoweza kutuokoa nje ya Damu ya Mwanao Yesu, Yeye ni Mwokozi wetu, tunampenda.

²¹⁰ Nasi tunajua ya kwamba uponyaji wa Kiungu ni Wako, ni mali Yako, kwa kuwa tunasoma katika Zaburi 103:3, “Mimi ni Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote.” Kwa hiyo, Bwana, tunakabidhi ugonjwa wetu Kwako, Wewe ndiwe Tabibu wetu, Tabibu wetu Mkuu.

²¹¹ Uko hapa usiku wa leo, watoto Wako waaminio wanalitii Neno Lako, kwa kuwekeana mikono, hapa ni kuanzia mhudumu kote kote hata wa—walei wa kanisa, kila mtu, wachungaji, wainjilisti wote wamewekeana mikono, mke wa nyumbani, watoto wote wamewekeana mikono, kwa sababu wanamwamini Huyu tunayemchagua, Bwana wetu, Mponyaji wetu.

²¹² Sasa, Shetani, unajua ya kwamba wewe ni . . . ? . . . na wewe si kitu ila mdanganyifu, kwa vyovyote vile, nasi tunakupa changamoto. Bwana wetu ameteuliwa moyoni mwetu, kama Mponyaji, kama Mwokozi, kama Mfalme, kama Mtawala. *Bwana*: “umilikaji, utawala.” Sasa itakubidi kutoka, Shetani,

afadhali ujitayarishe kwenda, kwa sababu huna budi kuondoka, Neno la Mungu halina budi kutimizwa.

²¹³ Kwa hiyo ninakuamuru, kwa Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, kupitia mateso Yake makali, na ushindi, Yule aliyekunyang'anya, ama, aliyekuvua kila haki ya kisheria uliyokuwa nayo, huna haki tena kisheria, wewe ni kiumbe kilichoshindwa, nasi tunakuapisha, kwa Yesu Kristo, toka ndani ya watu hawa, waache, kwa kuwa wamewekeana mikono. Katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani yao, ninawafungua kwa utukufu wa Mungu, katika Jina la Bwana Yesu.

²¹⁴ Vichwa vyenu vikiwa vimeinamishwa sasa. Mlihisi wema Wake ukiingia. Aminini, haidhuru linaonekana la kuchekesha jinsi gani. Hatuzingatii jinsi linavyoonekana la kuchekesha, tunazingatia jinsi lilivyo halisi, ni Neno la Mungu.

²¹⁵ Kwa namna fulani ni jambo la kuchekesha kwa Nuhu kusema itanyesha, bali i-ilinyesha. Kidogo ni la kuchekesha kwa Ibrahimu akiutafuta Mji, na kusema atapata mtoto alipokuwa na umri wa miaka mia moja, kwa Sara aliyekuwa na tisini, bali alimpata. Ni jambo la kuchekesha kwa Musa kusema anashuka kwenda Misri kuiteka, lakini aliiteka, Mungu alisema hivyo. Kwa namna fulani ni la kigeni kwa wana wa Kiebrania kusema, "Mungu wetu anaweza kutuokoa na tanuru hii ya moto," Naye alifanya hivyo.

²¹⁶ Danieli alitoka katika tundu la simba akiwa hai, baada ya kuwa mle ndani, simba wakali, wenye njaa, usiku kucha, bali alifanya hivyo. Yohana kutoka kwenye pipa la—pipa la mafuta baada ya kuchomwa moto kwa saa ishirini na nne, bali alifanya hivyo. Lazaro alitoka kaburini baada ya kufa kwa siku nne, lakini alitoka. Yesu alifufuka katika siku ya tatu baada ya kusulubiwa, na mwili huo ulichomwa na mkuki wa Kirumi. Shahidi wa duniani alisema, "Amekufa," Mungu akasema, "Amekufa," maumbile yakasema, "Amekufa," dunia ikasema, "Amekufa," Mrumi akasema, "Amekufa," kila kitu kilisema amekufa, Naye yu hai tena milele. Alikuwa anaenda kufanyaje jambo hilo? Lakini Yeye alilifanya.

²¹⁷ Mungu anakuponya sasa, ahadi Yake inasema anakuponya, kwa hiyo una haki kwake. Unaukubali? Je, unaukubali uponyaji wako? Sijali jinsi ulivyolemaa, jinsi ulivyo kipofu, jinsi, chochote kilicho shida yako, sijali. Naomba usimame kwa miguu yako sasa hivi, na kusema, "Ninakubali uponyaji wangu juu ya msingi wa Neno la Mungu." Simama kwa miguu yako, kama unaamini. Amina. Amina. Hilo ni zuri. Ajabu! Sasa, vema, sasa.

²¹⁸ Sasa, wewe ambaye hukuwa mgonjwa, na unataka kumkubali Yeye kama Bwana moyoni mwako, amini jukwaani, unayetaka kumchagua Yesu kuwa Mtawala wa uamsho huu, kuwa Mponyaji katika uamsho huu, kuwa Bwana katika uamsho huu, nyinyi wengine simameni kwa miguu yenu,

mtakaofanya hivyo, msemi, “Ninamkubali Yeye kuwa Bwana wangu, Mponyaji wangu, Yote kwangu (Mwokozi wangu) katika Yote katika uamsho huu.” Ajabu, kila mtu amesimama kwa miguu yao. Hilo ni sawa.

²¹⁹ Loo, ninaamini, ninasikia sauti ya mvua nyingi, wachungaji. Ninaamini kutakuwa na jambo fulani litakalotukia hapa. Ni wangapi wanaojisikia hivyo, wanaamini hilo? Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote.

²²⁰ Sasa hebu na tumsifu, tupe sa—sauti ya “Nampenda, nampenda.” Je, unaujua wimbo huo? Vema, kila mtu sasa, pamoja.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Hebu tuuvumishe sasa. Wokovu gani? Wokovu wa nafsi na mwili.

...alinipenda kwanza
Na kununua...

Msisahau saa kumi na mbili na nusu kesho usiku, kadi za maombi. Ninatarajia mambo makuu kutoka kwa Bwana.

Mtini...

²²¹ Tunapoinamisha vichwa vyetu, tutairudisha ibada kwa uamsho wetu, ama, meneja wenu, Ndugu Roy Borders. Kumbukeni kadi za maombi zitatolewa kesho usiku saa kumi na mbili na nusu, hapa ukumbini, na maombi kwa ajili ya wagonjwa yataanza kesho usiku. Vema, Bwana awabariki mpaka nitakapowaona tena. Ndugu Borders. 

60-0729 Kile Kinachohitajika Kushinda
Kutokuamini Kwote: Imani Yetu
Eisenhower High School
Yakima, Washington Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org